TRUTH CENTERED TRANSFORMATION

MODULE



# KUISHI KAMA MUNGU ANAVYOKUSUDIA

## MWONGOZO WA MWALIMU

Truth Centered Transformation is a ministry of Reconciled World. Learn more at tctprogram.org.

Reconciled World

Truth Centered Transformation—Moduli: Kuishi kama Mungu anavyokusudia v3. Copyright ©2018 Reconciled World, Phoenix, Arizona, United States of America. www.reconciledworld.org

Kazi hii inapatikana kwa kuzingatia masharti ya leseni ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 3.0. Unaruhusiwa na kuhimizwa kutumia kazi hii, kunakili, kusambaza, na kuitangaza kwa masharti yafuatayo:

**Nukuu** - Lazima unukuu kazi hii kwa kusema yafuatayo: Copyright © 2012 Published by Reconciled World (www.reconciledworld.org) under terms of the Creative Commons Attribution–ShareAlike 3.0 license. Kwa taarifa zaidi, angalia www.creativecommons.org.

**Kazi hii haiuzwi** - Usitumie kazi hii kwa sababu za kibiashara.

Ukiwa na nia ya kutafsiri matirio hii, tafadhali wasiliana na info@tctprogram.org.

Nukuu zote za maandiko matakatifu, zimechukuliwa kwenye Biblia Takatifu, toleo la New International Version®, NIV® Hakimiliki © 1973, 1978, 1984, 2011 by Biblica, Inc.TM. Ikitumika kwa ridhaa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa dunia nzima. www.zondervan.com. The "NIV" na "New International Version" ni alama za biashara zilizosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office na Biblica, Inc.TM.

# Yaliyomo

*Masomo katika Sehemu A ni kama saa 1 kila somo. Yanaweza kutumika kama somo la vikundi vidogo vya kila wiki kusaidia kuwafanya washiriki wa kanisa lako kuwa wanafunzi. Sehemu B inakusudiwa kusaidia kanisa zima kutathmini maendeleo yao tangu mwanzo wa programu ya TCT, kusherehekea yote ambayo Mungu amefanya, na kuweka mpango wa kuendelea kusonga mbele katika kuona mabadiliko. Ni vyema kupanga siku moja kamili ili kukamilisha sehemu mbili za Sehemu B.*


**SEHEMU A**

1**Somo la 1 : Kwa nini tumtii Mungu?**
1Utangulizi
1Kuelewa maana ya Wokovu
1Tunaokolewaje?
4**Somo la 2 : Tunatarajiwa Kufanya Nini?**
6Utangulizi
6Kuwapenda Jirani zetu
6Kufupisha Biblia
6Sababu za kutowapenda wengine
7**Somo la 3: Tunawezaje Kusaidia?**
9Kuwasaidia wengine
9**Somo la 4: Ufalme wa Mungu**
12Ufalme wa Mungu
12Kitabu chetu cha Maelekezo
12Kukua Kama Mungu Anavyokusudia
13**Somo la 5: Tumaini la Wakati Ujao**
15Injili nzima
16Kupatanisha Mambo Yote
17Jinsi ya kuwa Mjenzi wa Ufalme
19**Somo la 6: Tumia Kila Kitu Alichokupa Mungu**
20Hadithi Tatu za Biblia
21Mungu Huzidisha
24**Somo la 7: Fanya kazi ili Kumtukuza Mungu**
25Kwa nini Tunapaswa Kufanya kazi?
25Mungu anajali Jinsi Tunavyofanya Kazi Yetu
25Kilimo cha Kumtukuza Mungu
26**Somo la 8: Ukweli juu ya Shetani**
28Shetani ni Mwongo
28Ukweli wa Mungu Utatuweka Huru
30**Somo la 9: Kuwafunza Wengine**
32Agizo Kuu
33Uwe Mfano Mzuri kwa Wengine
33Kuwa Muwazi
34**Somo la 10: Kumletea Mungu Utukufu**
36Ukristo ni nini?
36Shadraka, Meshaki na Abednego
36Kuakisi/ Kuonyesha Utukufu wa Mungu
37**Somo la 11: Tufanyaje Mambo Haya Yote?**
38Utangulizi
39Kitabu cha Matendo
40**SEHEMU B:**

41**Kipengele cha 1: Tumetoka Mbali Kiasi Gani?**
41Tumetoka mbali kiasi gani?
41Mabadiliko ya Kawaida
44Kutumia Yale Tuliyojifunza
45Tunataka kwenda wapi?
46**Kipengele cha 2: Kusonga Mbele**
47Sehemu Zote Zimeunganishwa Pamoja
47Mafunzo
47Matendo ya Upendo
49Kukaa Ndani Yake
50Hatua ifuatayo ni ipi?
50

# Kabla ya kuanza

## Maandalizi ya Kufundisha Somo

1. Usome **Mwongozo wa Mwalimu** kwa uangalifu, mara nyingi iwezekanavyo. Weka alama au andika notsi chini ya mstari kujikumbusha hoja za muhimu.
2. Angalia **malengo makuu** ya kila somo ili ujue mwanafunzi anahitaji kujifunza nini katika somo.
3. Soma aya zote za **maandiko matakatifu** kabla.
4. Angalia ili uone **nyenzo** zipi zinahitajika katika kila somo na uandae Vioneshi ambavyo vinatumika katika somo. Unaweza kutoa nakala za Mwongozo mzima wa Wanafunzi kwa kila Kanisa ili kuwasaidia kurudia na kutumia kile ambacho wamejifunza. Usipotumia Mwongozo wa Mwanafunzi, unaweza kuandika mistari na maswali kwenye ubao mweupe au bango au kuandika mistari hiyo kwenye vipande vidogo vya karatasi kwa kila kikundi.
5. Hakikisha unaelewa kila **kitendo au shughuli** katika somo (maigizo, michezo, picha za kujifunzia/vioneshi). Unaweza kufanyia mazoezi na ndugu au marafiki.
6. Tumia muda **kusali au kuomba** ili Mungu awaandae wanafunzi, wasikie kile Mungu anachotaka wasikie, na ili akusaidie kufundisha matirio. Kumbuka kwamba ni kwa njia ya nguvu ya Mungu tu ambayo tutawaona watu wakibadilika

## Jinsi ya Kutumia Mwongozo huu wa Mwalimu

1. **Mawazo Makuu na Nyenzo:** Kila somo huanza na sehemu hii.
    a. **Mawazo Makuu**– Haya ni mawazo muhimu zaidi ambayo wanafunzi wanapaswa kuyaelewa kwa uwazi mwishoni mwa kila somo. Mwishoni mwa somo tumia muda wa kurudia kuhakikisha kuwa wanafunzi wameelewa mawazo haya.

    b. **Nyenzo** - Nyenzo mahususi zinazohitajika zimeorodheshwa kwa kila somo.
        i. **VIONYESHI** – vitaandikwa hivi. Vinapaswa kuchapishwa kabla ya wakati.
        ii. Tunapendekeza uwe na karatasi, ubao mweupe au ubao wa chaki wa kutumia na kundi kubwa.
        iii. Miongozo ya Wanafunzi ni ya hiari. Sehemu yoyote ya somo ambayo ina kurasa zinazolingana katika Mwongozo wa Mwanafunzi imeandikwa katika Mwongozo wa Mwalimu kama hii: (MW).

2. **Maelekezo ya Mwezeshaji:** Kuna maelekezo maalum katika somo kukusaidia uongoze mafunzo vizuri. Haya hayakusudiwi kutolewa kwa wanafunzi. Soma haya kabla ili ujiandae kuongoza majadiliano na shughuli. Baadhi ya maswali yatakuwa na majibu yaliyoitalikiwa (italicized) kukusaidia kama mwezeshaji ujue ni mawazo gani ya kuyasisitiza kwa wanafunzi. Haya si majibu sahihi pekee, bali ni baadhi tu ya majibu mazuri.

# SEHEMU A
# Somo la 1: Kwa nini Tumtii Mungu?

**Mawazo Makuu**

1. Yesu alitupenda sana Alikufa Msalabani ili achukue adhabu tuliyostahili.

2. Maisha yetu yanapaswa kubadilishwa tunapojua thamani na maana ya kifo cha Yesu Msalabani.

**Nyenzo**

1. Vionyeshi : Igizo la Mkristo Mpya (chapisha nakala moja na ukate katikati)
2. Mwongozo wa Mwanafunzi Hiari: Hadithi ya Jude (MW)

## Utangulizi

**SHUGHULI YA KUNDI KUBWA (IGIZO)**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:****Waombe watu 2 wa kujitolea waigize igizo lifuatalo (**VIONYESHI** Igizo).*

**Muumini wa Muda Mrefu***: Kwa kuwa sasa wewe ni Mkristo, unapaswa kusali, kusoma Biblia kila siku, kwenda kanisani, na kujiunga na kikundi kidogo ili kujifunza Biblia mara moja kwa juma. Lazima uache kuvuta sigara na kunywa pombe.*

**Muumini Mpya**: *Ni mambo mengi sana! Nilifikiri nilihitaji tu kuomba na kuamini ili nipate kuokolewa. Ndivyo ulivyosema hapo awali!*

**Muumini wa Muda Mrefu:** *Ndiyo, lakini sasa lazima ufanye mambo mengine yote pia.*

**Muumini Mpya:** *Kwa nini? Nadhani tayari nimeshaokoka. Nataka kwenda mbinguni, hivyo tu. Sitaki kubadilisha jinsi ninavyoishi.*

**MAJADILIANO YA KUNDI KUBWA**

- Nani yuko sahihi katika igizo hili? Je, ni lazima tufanye mambo mengi au tuombe na kuamini ili tupate kuokolewa?
- Ungekuwa muumini wa muda mrefu, ungemwambia nini mwamini mpya?
- Je, umewahi kukutana na muumini anayefikiria hivyo?

## Kuelewa Maana ya Wokovu

**MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO**
***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Soma hadithi hii na uwape vikundi vidogo maswali ya majadiliano.* (MW)

Sikiliza Hadithi ya Yuda. Jibu maswali katika vikundi vyako vidogo na kisha shirikisha majibu yako na kikundi kikubwa.

Hadithi ya Yuda:

Kila mtu kijijini alijua yeye ni mwovu. Yuda alikuwa mshirika wa genge na mlevi. Hakuna mtu aliyeweza kukumbuka kabisa kuwahi kumuona akiwa mzima, alikuwa amelewa kila wakati. Alimnyanyasa mke na watoto wake, hakuwahi kusaidia shambani na aliogopwa na watu wengi. Alibeba kisu na kuwaibia watu kwa kukitumia kisu. Akiwa katika hali mbaya alichoma nyumba za watu. Polisi hawakuwa na msaada; walimwogopa pia. Hakukuwa na kitu mtu yeyote angeweza kufanya. Wote walimkwepa.

Lakini sasa alikuwa amefanya hivi. Yuda alikuwa ameua mtu - mchungaji zaidi! Kulingana na wale walioona, Mchungaji Mathayo alikuwa amemaliza tu mkutano wa kanisa na alikuwa akielekea nyumbani. Alilifunga jengo lile huku akipiga mluzi wimbo waliokuwa wametoka kuuimba kanisani huku akielekea nyumbani kwake umbali wa mita mia chache tu. Yuda alikuwa akinywa bia yake na alionekana kukasirika haraka kwa mluzi wa mchungaji. Alimshambulia Mchungaji Mathayo kwa kisu na kukimbia. Kila mtu kwenye baa hiyo aliharakisha ili kumsaidia mchungaji lakini walipomfikisha Mathayo hospitalini, umbali wa maili 20, alikuwa amekufa.

Mazishi yalikuwa ya kusikitisha sana. Mkewe alikuwa na watoto saba, wenye umri wa miaka 2 hadi 15. Hakuweza kuacha kulia. Ingawa alijua kwamba mume wake alikuwa mbinguni pamoja na Kristo, alilemewa na hali ya kutokuwa na tumaini. Je, angewezaje kuwalisha watoto wake? Wangewezaje kuishi? Kanisa lilisaidia lakini wote walikuwa wakulima maskini. Alijua ndani ya miezi michache zawadi za ukarimu za mchele na pesa kutoka kwa wale wa kanisani zingekauka na angebaki bila chochote isipokuwa deni la mazishi. Alimtazama Thomas mtoto wake mkubwa. Alikuwa mvulana mzuri sana, aliye tayari na mwenye hamu ya kusaidia hata marafiki zake walipotaka tu kucheza lakini ni kiasi gani angetarajia kutoka kwake. Alimshukuru Mungu kwa kuwa Thomas alikua ni kijana mzuri na kumuomba Mungu amtie nguvu kwa kazi ngumu ya kuwa mwanaume katika familia hiyo kwa sasa.

Yuda aliishi kama mkimbizi. Miezi michache baada ya mauaji hayo watu katika kijiji hicho walisikia kwamba ameua mtu mwingine katika kijiji kilicho umbali wa maili 10 na baadaye mtu mwingine katika kijiji tofauti. Mke wa Yuda kwa nadra alitoka nyumbani kwake, aibu yake ilikuwa kubwa. Mara kwa mara polisi walikuwa wakija na kumsumbua, wakimwuliza Yuda yuko wapi. Lakini kila mtu alitambua kuwa alikuwa mhanga pia. Alikuwa ameachwa na alipambana kuishi. Kwa kweli halikuwa kosa lake kwamba Yuda alikuwa mwovu sana.

Jude alipokuwa akiua mtu wa tano katika mji mkuu wa wilaya, alikamatwa. Ilichukua chini ya siku moja kwa kila mtu kusikia kukamatwa kwake. Kesi ilipangwa na uvumi ulikuwa kwamba atahukumiwa kifo. Mada ilijadiliwa kila mahali, kwenye kisima cha jamii, mashambani, majumbani. Yuda alikuwa anaenda kufa. Kila mtu alikubali, hakika alistahili. Alimwua mchungaji wao na wanne wengine. Hakika alikuwa mtu mwovu. Lakini bado ilikuwa vigumu kufikiria kwamba mmoja wao angeenda mahakamani na angekufa.

Kundi kutoka kijiji kiliamua kuhudhuria kesi ambayo ingefanyika katika mji mkuu wa mkoa. Wachache walikuwa hata wameombwa kutoa ushahidi juu ya mauaji ya Mchungaji Mathayo. Kulikuwa na mkanganyiko kidogo kwani kila mmoja alifanikiwa kuazima nguo zinazostahili kwa ajili ya tukio hilo muhimu na mipango ya safari hiyo ndefu ikafanywa. Ilikuwa ni kitulizo kujua kuwa hatimaye haki ingetendeka. Yuda alikuwa mwovu kweli.

Siku ya kesi ilikuwa ya joto, joto sana. Chumba kidogo kilikuwa na watu wengi wakishangaa. Hakimu aligonga meza kwa nguvu ili watu watulie. Kukawa kimya mara moja. Yuda alisimama kwenye kizimba cha uhalifu akimwelekea hakimu. Hakimu aliinua karatasi zake na kusoma mashtaka dhidi yake. "Uko hapa kwa kesi ya mauaji ya watu wanne" - na alisoma majina. “Unasihi vipi?” Yuda alikana mashitaka. Siku iliendelea huku mashahidi wa kila mauaji yale manne wakinyanyuka na kueleza walichokiona. Mara nyingi mashambulizi hayo hayakuchochewa. Watu walikuwa wakifanya mambo yao wakati Yuda alipowaua. Katika kisa kimoja tu yalikuwa mapigano yaliyokuwa yameanza wakati wanakunywa pombe. Chupa zilikuwa zimerushwa na mtu akafa.

Joto ndani ya chumba cha mahakama lilizidi kutanda na maelezo ya mauaji yale yalimfanya kila mmoja ajisikie vibaya kidogo. Lakini walipokula chakula cha mchana wote walikubaliana jambo moja. Yuda alistahili kufa.

Baada ya chakula cha mchana walirudi tena chumbani. Walipokaa wote na kutulia hakimu aliingia chumbani. Alionekana tofauti kwa namna fulani, laini kidogo labda. Aliwanyamazisha na kuanza kuongea.

“Yuda, nimezingatia kesi yako na bila shaka una hatia na unastahili kifo. Haki lazima itendeke.” Chumba kilikuwa kimetulia kwa uchungu. Huu ulikuwa wakati; huu ulikuwa wakati ambao Yuda alikuwa anaenda kuhukumiwa kifo. “Hata hivyo, pia nimepokea ombi maalum, ombi ambalo nimelizingatia. Ombi nimeamua kulikubali.” Maafisa wengine wa mahakama walitazamana, wakiwa wamechanganyikiwa. Wale waliokuwa kwenye hadhira waliona mkanganyiko wa maafisa wa mahakama pia walianza kunung'unika wenyewe kwa wenyewe. "KIMYA." Chumba kilikuwa kimya mara moja, kelele zilizosikika ni zile za feni zikizungusha joto chini kutoka kwenye dari. Watu walipumua kwa tabu.

“Yuda, mjane wa Mathayo amenitembelea na kuuliza kwamba badala yako wewe, mwanawe, Thomas, ungelipa gharama. Nimezungumza na Thomas na mjane wa Mathayo kwa kirefu na kukubaliana na ombi lao. Yuda, una hatia ya mauaji yote manne. Thomas, utahukumiwa kifo kwa mauaji hayo manne. Yuda uko huru kuondoka.” Naye akapiga goti lake.

Kelele na mkanganyiko ulitokea mara moja. Kwa muda mfupi hakuna aliyezungumza kisha kila mtu alizungumza kwa mara moja. Thomas alikuwa anaenda kufa kwa ajili ya mauaji ya Yuda. Ilikuwa mbaya sana, haikuwa haki. Thomas alikuwa mvulana mzuri sana. Alifanya kazi kwa bidii kumtunza mama yake tangu kifo cha baba yake. Hakuwahi kufanya jambo lolote baya. Yuda alikuwa mwovu na ulimwengu ulihitaji kumwondoa. Wachache walimwangalia Yuda, alipokuwa amekaa sakafuni akilia.

- Yuda alipokeaje yale Thomas na mama yake waliyofanya?
- Unafikiri Yuda anaweza kubadilikaje kutokana na hili?
- Je, hadithi hii inahusiana vipi na sisi kama Wakristo?

**TOA RIPOTI**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Jadili seti ya kwanza ya maswali* (MW)*. Kisha soma seti ya pili ya maswali, na waache washiriki watafakari kibinafsi. Maliza kwa kuhakikisha kuwa kikundi kinaelewa mambo makuu hapa chini.*

Kwa wazi, hadithi hii sio kweli. Tunapoisoma mwisho haina maana. Haiwezekani kabisa. Lakini fikiria ikiwa kitu kama hiki kilitokea - mtu asiye na hatia alikufa kwa ajili ya dhambi za mwingine. Isingekuwa na maana. Isingekuwa haki. Na bado ilitokea. Yesu, ambaye hakutenda kosa, alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Alienda msalabani na kustahimili kifo cha kutisha sana kinachoweza kuwaziwa, kifo cha kusulubiwa. Hakustahili kufa. Hakuwa na hatia. Na bado alikufa ili kulipia gharama ya dhambi zetu.

Biblia inatuambia kwamba wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na viwango vya Mungu. ( Warumi 3:23 ) Sisi sote tunastahili kifo. (Warumi 6:23) Katika hili hatumaanishi kufa tu bali kwenda motoni milele. Kuteseka kwa milele. Hatuwezi kuondoa dhambi zetu kwa kuwa wema au kufanya mambo mema. Mtu anapaswa kulipia dhambi. Mungu alitupenda sana hata akamfanya mwanawe alipe gharama. Yesu alikufa kifo cha kweli na chenye uchungu kwa ajili ya dhambi zetu. Sasa, tukikubali zawadi hiyo, malipo hayo ya dhambi zetu, hatuhitaji kwenda kuzimu lakini tunaweza kuungana naye mbinguni.

**TAFAKARI BINAFSI**

- Je, umekubali zawadi hiyo?

- Unachaguaje kuishi kwa njia tofauti?
- Unadhani ni nini kingine kinahitaji kubadilika katika maisha yako kwa kuitikia zawadi ya Kristo?

Je, umeikubali zawadi ya kifo cha Kristo? Bila kukubali kifo cha Kristo tutaishi milele kuzimuni. Ikiwa tumeikubali zawadi hiyo basi tunapaswa kujiuliza swali hili -Mapokeo yetu yanapaswa kuwaje? Hebu tumkumbuke Yuda kwa muda. Je, aendelee kama kawaida - kunywa na kuua kama hapo awali? La, tungetarajia Yuda aishi maisha yanayostahili; kuacha pombe, kumtendea mke na watoto wake mema, kuwahudumia, kusaidia jamii. Amepewa nafasi nyingine maishani; anapaswa kuitumia vizuri kama kitendo cha shukrani kwa Thomas ambaye alilipa gharama kubwa. Tungeshtuka ikiwa Yuda angeendelea kuishi kama alivyokuwa siku zote.

Vipi kuhusu sisi? Tunaishi vipi? Je, tunaishi kama watu wanaotambua kwamba Yesu alikufa kifo cha uchungu ili kutupa nafasi ya pili? Je, tunaishi tukijua kwamba tunapendwa kiasi hicho? Je, tunaishi kuheshimu dhabihu hiyo? Je, tunaishi kwa shukrani? Mungu ametuambia katika Neno lake jinsi anavyotutarajia tuishi. Kuwa mtiifu hakutatuokoa. Lakini tunapaswa kuwa watiifu kwa sababu tunatambua gharama kubwa iliyolipwa kwa ajili yetu. Kwa sababu tunataka kumwonyesha Mungu jinsi tunavyoshukuru sana kwa ajili ya dhabihu yake.

Lakini Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi katika hili: Tulipokuwa bado wadhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu (Warumi 5:8).

## Tunaokolewaje?

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Waefeso 2:8-10.

- Tunaokolewaje? (Mstari wa 8)
- Tunapaswa kufanya nini kama matokeo ya kuokolewa kwa njia hii? (Mstari wa 10)
- Unafikiri ni nini maana ya maneno “kwamba hakuna awezaye kujisifu”? (Mstari wa 9)

Hatuwezi kutimiza wokovu wetu wenyewe kwa kufanya matendo mema. Tunategemea kabisa neema ya Mungu. Neema yake ni zawadi na haiwezi kununulika. Kwa kuwa ni zawadi, hatuwezi kujivunia au kudai sifa yoyote. Hakuna hata mmoja wetu anayefikia kiwango cha Mungu. Ni lazima tumtegemee Mungu atuokoe.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Andika sentensi zifuatazo ubaoni.*

**HATUOKOLEWI KWA KUJIBADILISHA. TUNABADILISHWA KWA SABABU TUMEOKOKA.**

Kuna tofauti gani kati ya sentensi hizi mbili?

- *Mungu alituokoa. Haya si matokeo ya juhudi zetu wenyewe.*
- *Tunapoelewa zawadi ya Mungu kwetu, basi tunaitikia kwa kuishi tofauti ili kumpendeza.*

Fikiria wakati ulipoguswa na wema wa mtu mwingine kwako.

- Ulifanya nini kutokana na hilo? Uhusiano wako na mtu huyo ulibadilikaje?
- Je, ulilazimishwa kuwalipa au ulitaka tu kuwalipa kutokana na wema wao?
- Hii inamaanisha nini kuhusiana na mwitikio wetu kwa Kristo kama tokeo la zawadi yake ya wokovu?

- *Ni lazima tufanye mambo mema kutoka moyoni, si kwa sababu ya wajibu. Hili lazima litokee tunapoelewa thamani ya Msalaba. Ni lazima tubadilike, si kwa sababu tunalazimishwa kufanya hivyo, bali kwa sababu tunataka kumpendeza Mungu na kuonyesha shukrani zetu kwake.*

**MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO**

Katika vikundi vidogo, jadili swali lifuatalo na utengeneze orodha ya majibu.

- Ni kwa njia gani maisha yetu yanapaswa kubadilika kama matokeo ya zawadi ya Kristo?

**TOA RIPOTI** kwenye kundi kubwa

**UTUMIAJI WA TAARIFA**

Kutoka kwenye orodha ya mawazo, chagua jambo moja unalopenda kuona likibadilishwa maishani mwako ili kuonyesha upendo wako kwa Mungu. Unawezaje kujikumbusha kila siku kuendelea kufanya mabadiliko hayo maishani mwako?

**MUHTASARI**

Angalia maisha yako. Kwa sababu wewe ni Mkristo, je, maisha yako ni tofauti? Je, yanapaswa kuwa tofauti na wale ambao bado hawajamwamini Mungu? Kwa nini?

Katika masomo yafuatayo, tutaona kile Mungu anachotarajia kutoka kwetu. Tunahitaji kukumbuka kwamba tunataka kukidhi matarajio haya si ili tupate wokovu, bali kwa sababu tunashukuru kwamba tayari ameshatuokoa.

# Somo la 2: Tunatarajiwa Kufanya Nini?

**Wazo Kuu**

1. Ni amri gani ambayo Paulo anasema inafupisha torati yote na manabii? Sheria yote na manabii wamefupishwa wakisema "Mpende jirani yako." Tunahitaji kufanya hili katika maisha yetu.

**Nyenzo**

1. Vioneshi: Kuonyesha chati ya Upendo – nakala 1 kwa kila kikundi kidogo
2. Mwongozo wa Mwanafunzi hiari (MW)
    a. Kuonyesha Jedwali la Upendo.

## Utangulizi

**MAJADILIANO KATIKA KIKUNDI KIDOGO**

- Mungu anatarajia nini maishani mwetu? Ikiwa mwamini mpya atakuuliza swali hili, ungejibuje?

Katika masomo yafuatayo tutajifunza majibu mbalimbali kwa swali hili – "Tunawezaje kuishi kama Mungu anavyokusudia?" Tunavyojaribu kuishi tofauti tunahitaji kukumbuka sababu. Hatujaribu kuishi tofauti ili tuokolewa. Badala yake, tayari tumeshaokolewa tunapompokea Kristo kama Mwokozi wetu. Tunataka kuishi kwa njia tofauti kulingana na yale aliyotufundisha ili tuonyeshe upendo na shukrani zetu kwake.

## Kuwapenda Jirani Zetu

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Luka 10:25-37.

- Kinatokea nini katika hadithi?
- Kulingana na hadithi hii, jirani yako ni nani?
- Hadithi hii inatuonyeshaje namna ya kumpenda jirani yetu?
- Yesu alikuwa akijibu swali gani? (Mstari wa 25)

Soma Marko 10:17-21.

- Swali la kijana tajiri ni lipi?
- Jibu la Yesu ni lipi?

Kwa mara nyingine tena tunaona kwamba sehemu ya jibu la kuwa Mkristo ni kwamba lazima tuwasaidie wasiojiweza. Inaweza kuhitaji dhabihu/sadaka yetu lakini Yesu ametuonyesha wazi kwamba hii ni sehemu muhimu ya kumfuata Mungu.

Soma 1 Wakorintho 13:1-3.

- Mistari hiyo inatufundisha nini?
- Tunahitaji kufanya nini? (UPENDO!)

Hapa Mtume Paulo alionyesha kwamba tunaweza kufanya mambo mazuri mengi, lakini ikiwa msukumo wetu sio UPENDO basi yote hayana thamani.

## Kufupisha Biblia

**MJADALA WA KUNDI KUBWA**

Katika somo letu la kwanza kabisa la mafunzo tulijifunza jinsi ya kufanya muhtasari / ufupisho wa Biblia nzima. Soma Mathayo 22:36-40.

- Amri mbili muhimu zaidi ni zipi?
- Iwapo amri moja tu ingetumiwa kufupisha Biblia, unafikiri ingekuwa ipi?

Soma Wagalatia 5:14.

- Ni amri gani ambayo Paulo anasema inafupisha torati yote na manabii?
- Unadhani kwa nini Paulo anachagua amri hii badala ya amri nyingine (kumpenda Mungu)?

Ikiwa tumeokolewa kwa neema, basi kwa nini msisitizo zaidi unatolewa kwa mambo tunayowafanyia jirani zetu? Inaonekana haina mantiki. Daima hufundishwa kwamba hatuokolewi kwa yale tunayofanya, bali tu kwa yale ambayo Yesu amefanya. Kwa hiyo, kwa nini mara nyingi tunaona kwamba Biblia inasisitiza umuhimu wa kuwapenda wengine?

Soma 1 Yohana 5:3 na Yakobo 1:27.

- Mistari hii inatusaidiaje kuelewa kwa nini ni muhimu kuwapenda wengine?
    - *Kuwapenda wengine ndiyo njia tunayoonyesha shukrani zetu kwa Mungu. Ni kama jaribio la kuona kama mtu ni Mkristo wa kweli. Maisha ya Mkristo halisi yanabadilika kweli. Yohana na Yakobo walipendekeza njia ya kujua kwa kuangalia jinsi tunavyotii amri za Mungu na kuwatendea wengine.*

Watu wanaweza kujua sisi ni Wakristo kwa jinsi tunavyowapenda wengine.

## Sababu za kutowapenda wengine

**MAJADILIANO YA KIKUNDI KIKUBWA**

Angalia tena Luka 10:25-37.

Njia ya kutoka Yeriko ni ngumu sana na hatari. Iliitwa "njia ya Damu." Yerusalemu iko mita 750 juu ya usawa wa bahari na Yeriko iko mita 260 chini ya usawa wa bahari. Hii inamaanisha ni mwinuko sana - tofauti ya zaidi ya mita 1000 katika mwinuko, lakini ni kilomita 25 tu kwa umbali kati ya miji miwili.

Watu wawili walimpuuza mwathiriwa. Tunawahukumu, lakini kuwa makini, kwa sababu sisi ni wepesi wa kufanya kosa lilelile. Barabara ya kuelekea Yeriko ilikuwa hatari sana - Wangesimama kusaidia mwathiriwa, wangeweza pia kuwa mwathirika wa pili wa wezi. Wana sababu ya kutosaidia. Na sisi ni kama wao pia. Tunatoa sababu nyingi za kutosaidia, kama vile kuogopa sana.

- Baadhi ya sababu gani tunazotoa mara nyingi za kutowasaidia maskini au wahitaji?

**MAJADILIANO YA KIKUNDI KIDOGO** (MW)

Katika vikundi vidogo, jaza jedwali la **Kuonyesha Upendo** (**VIONESHI**)**.**

*Fikiria watu tofauti walioorodheshwa hapo chini. Kwa kila moja, jaribu kufikiria mtu mahususi anayelingana na maelezo hayo, kisha andika jambo moja unaloweza kufanya ili kuonyesha upendo kwa mtu huyo. Ukimaliza, chagua angalau watu 2 kutoka kwenye orodha na ujitolee kufanya jambo wiki hii ili kuwaonyesha upendo.*

| **Jirani Zetu** | **Unawezaje Kuonyesha Upendo** |
|---|---|
| Mtu usiyemfahamu au mgeni katika jamii yako | |
| Mtu aliye kwenye migogoro na wewe | |
| Mtu aliye mbali na Mungu mf.mlevi, muuza madawa ya kulevya, mshirika wa makundi mabaya, n.k . | |
| Mtu aliyekuwa akienda kanisani, lakini haendi tena. | |
| Muumini mpya | |
| Rafiki | |
| Mshirika mwingine wa kanisa | |

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Maliza kwa vikundi vidogo kuombeana ili kutimiza ahadi zao za kuonyesha upendo wiki hii.*

# Somo la 3: Tunawezaje Kusaidia?

**Wazo Kuu**

1. Jifunze jinsi ya kuwasaidia wengine kwa namna ambayo hawatakuwa tegemezi kwetu.

**Nyenzo**

1. Mwongozo wa Wanafunzi Hiari (MW): Bi. Lee

## Kuwasaidia Wengine

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Mathayo 25:31-46.

- Kuna tofauti gani kati ya kondoo na mbuzi?
- Ni mambo gani sita ambayo kondoo walifanya?

Mungu anatuomba tuwatunze wahitaji. Katika somo hili tutajifunza zaidi juu ya njia bora zaidi tunayoweza kuwatunza.

Soma Ruthu 2:1-16

- Boazi alimfanyia nini Ruthu?
- Unafikiri kwa nini Boazi alimsaidia Ruthu kwa njia hii badala ya kumpa chakula tu?
    - *Boazi alimruhusu Ruthu kukusanya nafaka mwenyewe ili apate heshima ya kufanya kazi na kuweza kumsaidia mama mkwe wake.*

Kuna tofauti muhimu kati ya vifungu hivi viwili (Mathayo 25:31-46 na Ruthu 2:1-16). Ya kwanza ni mfano wa kutoa "vitu vya muda mfupi." Ya pili ni mfano wa kuhudumia "msaada wa muda mrefu." Ni muhimu kuelewa tofauti kati ya vitu vya muda mfupi na msaada wa muda mrefu na ni kwa hali gani kila moja inafaa zaidi.

- **Kutoa msaada/vitu vya muda mfupi** vinafaa zaidi katika hali za dharura za muda mfupi. Mifano ni pamoja na nyumba ya mtu inapoungua, mtu anaugua ghafla, au kuna maafa ya asili kama mafuriko, kimbunga, au maporomoko ya ardhi. Mathayo 25:31-46 inazungumza zaidi juu ya msaada wa muda mfupi kama vile kutoa chakula, maji, malazi, mavazi, n.k.
- **Msaada wa muda mrefu** unafaa zaidi kwa matatizo ni sugu, ikimaanisha kuwa hayajabadilika au kutatuliwa kwa muda mrefu sana. Mifano ni pamoja na familia inapokosa chakula kila mwaka au kuingia madeni, au watu wanapougua kila mara magonjwa yale yale. Msaada wa muda mrefu unahitajika matatizo yale yale yanapoendelea kutokea mwaka baada ya mwaka. Ruthu 2:1-16 ni mfano wa msaada wa muda mrefu. Boazi hakutoa msaada wa chakula, bali badala yake alimpatia Ruthu kazi aweze kujipatia chakula.

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO** (MW)

Njia bora ya kusaidia wahitaji sio tu kuwapa chakula kila wakati. Hebu tusome mfano mwingine wa msaada wa muda mrefu. Bi. Lee ni mwanamke halisi. Anatamani kusaidia familia maskini katika jamii yake, haswa wale wasio na kazi. Anaanza kutembelea baadhi ya familia kila mwezi kutafuta njia za kuwasaidia kujikimu kimaisha. Hapa kuna hadithi tatu kati ya nyingi za jinsi ambavyo ameweza kusaidia familia. Hadithi hizi zote ni za kweli.

**Hadithi ya 1 – Bi. Lee na bustani ya maua**

Katika eneo lake, kulikuwa na familia maskini yenye watoto wawili. Mama na baba wote hawakuwa na kazi. Bi. Lee alipita kuwatembelea na akagundua kulikuwa na kipande kidogo cha ardhi chenye udongo mbele ya nyumba yao. "Kwa nini usipande maua," aliuliza. "Unaweza kuipendezesha nyumba yako kuwa nzuri zaidi na pia kuyauza kwenye soko lililo karibu."

Mama katika familia hiyo alifanya hivyo, na kuanza kupeleka sokoni maua aliyoyakuza na kuyauza. Mara aligundua kwamba wanunuzi walikuwa wakiulizia aina nyingine za maua pia, lakini alikuwa na kipande kidogo cha ardhi na hakuweza kupanda aina nyingine yoyote. Mama huyo, hata hivyo, alianza kununua maua kutoka kwa wakulima wengine na kuyauza, pamoja na yake, kwa faida. Sasa kwa kuwa alikuwa na nafasi ndogo sokoni ya kuuzia maua yake, alijisemea moyoni, “Ningeweza kuuza vitu vingine pia!” Yeye huamka mapema kila asubuhi kununua ndizi na nazi ili kuziuza sokoni kwenye sehemu yake anayouzia maua yake.

**Hadithi ya 2 – Bi. Lee na Viazi vitamu**

Familia nyingine iliyohitaji msaada ilitaka kufanya kazi, lakini haikujua la kufanya na haikuwa na ujuzi wowote maalum. Walifanya kazi kama vibarua wa kila siku, lakini mara nyingi hawakuweza kupata kazi. Bi. Lee aliweza kuona kwamba familia hii ilifanya kazi kwa bidii na ilitaka sana kufanya kazi, kwa hiyo alienda kutembelea familia nyingine kanisani waliokuwa wakulima wa viazi vitamu. Aliwauliza kama kilimo cha viazi vitamu kilikuwa na faida, kama kuna soko zuri, na vitu vinavyohitajika ili kuanza kilimo cha viazi vitamu.

Alipojua kwamba hiyo ilikuwa kazi nzuri, aliieleza familia hiyo kwamba Mungu ametuita tuwapende jirani zetu na kuwatunza maskini. Aliwaomba kama wangekuwa tayari kuifundisha familia maskini jinsi ya kuwa wakulima wa viazi vitamu. Walikubali. Bi. Lee alizitambulisha familia hizo mbili. Familia maskini ilifurahi kwamba sasa wangeweza kufanya kitu na haraka wakaenda kukodi kipande kidogo cha ardhi na kila kitu kilichokuwa muhimu kuanzia. Mwishoni mwa mwaka, walikuwa na mavuno mazuri na waliweza kulipa kodi ya shamba, pesa za mbegu, na bado walikuwa na faida nzuri kwa ajili ya familia.

**Hadithi ya 3 – Bi. Lee na upatanisho wa familia**

Familia ya tatu Bi. Lee alitaka kuisaidia ilikuwa imetengwa na wazazi wao. Wazazi waliamini kuwa familia hii haikuwa na maana na isingekuwa na chochote. Bi. Lee alikutana na familia ili ajaribu kuwapatanisha pande hizo mbili. Bi. Lee alihakikisha kwamba angekutana mara kwa mara na familia hiyo na kuwasaidia kuboresha maisha yao ikiwa wazazi wangekuwa tayari kuipokea familia hiyo na kuwasaidia kidogo. Kutokana na hali hiyo, wazazi waliamua kumwamini tena mtoto wao wa kiume na kuamua kumkopesha fedha ili aanzishe biashara ya vyuma chakavu. Sasa ananunua vitu vya zamani, vilivyotumika ambavyo vimetengenezwa kwa chuma na kuviuza kwenye duka la ndani la kuchakata upya. Sasa ana uwezo wa kuhudumia familia yake na anahisi mwenye heshima.

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO (VIONYESHI)**

- Bi. Lee alifanya nini kwa kila familia?
    - *Alitoa ushauri na kuwatia moyo*
    - *Alitembelea wengine, kama vile familia iliyolima viazi vitamu, ili kujua kama ilikuwa na faida na kama wangekuwa tayari kusaidia.*

- Matokeo ya vitendo vya Bi. Lee yalikuwa yapi?
    - *Watu walikuwa na kazi na waliweza kutunza familia zao.*
    - *Watu walijivunia kwa sababu walikuwa na uwezo wa kufanya kitu fulani ili kujisaidia.*

- Kingetokea nini kama Bi. Lee angetoa tu pesa au chakula kwa kila mmoja wa watu hawa?
    - *Wasingebadilika.*

- Bi. Lee angewapa pesa kila wiki kwa miaka miwili na kuacha, unafikiri maisha yao yangeboreka kama walivyofanya?
    - *Hapana, wangezoea Bi. Lee kuwapa pesa na wangetegemea hilo badala ya kufanya kazi.*

- Kuna tofauti gani kati ya kusaidia kwa pesa na jinsi Bi. Lee alivyosaidia?
    - *Aliwapa watu ujuzi na njia ya vitendo ya kujisaidia.*

- Fikiria kama wengi wetu tungeanza kufanya kama Bi. Lee—kutembelea familia na kusikiliza, kuangalia na kujaribu kuelewa matatizo yao, na kisha kutafuta suluhu. Jamii yako ingekuwaje?

**TOA RIPOTI**

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Matendo ya Bi. Lee yalikuwa mfano wa msaada wa muda mrefu. Hakuwapa tu familia chakula, alifanya kazi kutatua tatizo la muda mrefu. Ni muhimu kukumbuka kwamba msaada wa muda mfupi unafaa zaidi katika hali za muda mfupi, na msaada wa muda mrefu unafaa zaidi kwa matatizo ya muda mrefu.

- Fikiria Matendo ya Upendo ambayo kanisa lako hufanya. Je, mambo ya muda mfupi au msaada wa muda mrefu?

Katika programu ya TCT tumegundua kuwa jumuia hubadilika zaidi makanisa yanapoanza kushughulikia matatizo ya muda mrefu zaidi. Kujenga barabara, kukarabati shule, kuboresha kilimo, na kufundisha ujuzi kuhusu afya na usimamizi wa pesa ni njia za kushughulikia matatizo ya muda mrefu.

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO**

Orodhesha mambo 6 ambayo kondoo walifanya katika Mathayo 25:31-46. Gawa moja kwa kila kikundi. Waambie watengeneze orodha ya njia ambazo wangesaidia ikiwa matatizo haya yangekuwa ya muda mrefu katika jumuia yao. Kwa mfano, badala ya kuwapa chakula cha mara moja, ungesaidiaje familia ambazo mara kwa mara hazikuwa na chakula cha kutosha katika jamii yako? Au, badala ya kutoa dawa tu kila wakati, ungewasaidiaje watu wanaougua kila mara katika jamii yako, hasa kutokana na magonjwa yanayoweza kuzuilika kama minyoo na kuhara? Hamasisha vikundi kutoa njia chache za muda mrefu za kushughulikia kila hali.

**TOA RIPOTI**

# Somo la 4: Ufalme wa Mungu

**Mawazo Makuu**

1. Tunahitaji kuishi kwa utii kwa Mungu katika maeneo yote ya maisha yetu.

**Nyenzo**

1. Vionyeshi:
    a. Mchezo wa Mafumbo (Seti moja kwa kila kikundi chapisha kwenye kadi yenye chati ya namba upande mmoja na mstari wa Biblia upande mwingine. Kisha kata katika miraba na toa seti moja kwa kila kundi.
    b. Maelekezo ya Mchezo wa Fumbo (nakala moja kwa kila kikundi)
    c. Jedwali la Utamaduni Wetu na Biblia (nakala moja kwa kila kikundi)
2. Kadi Ndogo Tupu
3. Mwongozo wa Wanafunzi Hiari (MW)
    a. Jedwali la Utamaduni Wetu na Biblia

## Ufalme wa Mungu

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Luka 4:43.

- Kwa nini Yesu alitumwa?
- Ufalme wa Mungu ni nini?

Soma sala katika Mathayo 6:9-13.

Katika sala hii, tunasali kwamba "Ufalme Wake uje, Mapenzi Yake yafanyike duniani kama huko mbinguni." Je, unawezaje kueleza maana ya hiii kwa mtu ambaye si Mkristo?

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Sikiliza majibu kutoka kikundi. Baada ya kusikiliza, hakikisha wanaona kwamba maelezo lazima yaseme kutii mapenzi ya Mungu. Katika sala hii, tunasema tuko tayari kutii mapenzi ya Mungu katika maeneo yote ya maisha yetu hapa duniani kama tutakavyofanya mbinguni.*

Mungu anataka kuuona ufalme wake duniani kama ule wa mbinguni. Yesu na mtume Paulo mara nyingi hutaja ufalme wa Mungu lakini wachache wetu tunaelewa ufalme wa Mungu ni nini. Kwa kweli, wazo la ufalme wa Mungu si gumu sana kuelewa. Ufalme wa Mungu ni mahali popote ambapo Yesu ni Mfalme na sheria zake zinafuatwa. Kwa hiyo, ufalme wa Mungu unaonekana mahali popote tunapowaona watu wakiishi kwa kutii mapenzi ya Mungu. Kwa wazi, ufalme wa Mungu hautakuja kabisa hadi Yesu arudi na kila kitu kifanywe upya na hakutakuwa na dhambi.

Kuwa Wakristo ina maana kuwa tunahitaji kutembea katika utiifu wa Mungu katika maeneo yote ya maisha yetu.

## Kitabu chetu cha Maelekezo

**SHUGHULI YA KIKUNDI KIDOGO**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Kipe kila kikundi seti moja ya vipande vilivyokatwa kwa ajili ya mchezo wa mafumbo* ***(VIONYESHI:*** **Mchezo wa Mafumbo*)***. *Usiwape maelekezo kwanza. Wape dakika 3* ***tu*** *ili kuweka vipande vya mafumbo pamoja na* ***si zaid****i. Itakuwa vigumu sana kumaliza fumbo katika muda huu lakini wazuie baada ya dakika 3.*

*Kisha kipe kila kikundi Maagizo ya Mchezo wa Fumbo (****VIONYESHI: Maelekezo****). Wape dakika 3 zaidi kumaliza.*

1. *Geuza kila mraba wa karatasi kuonyesha namba. Weka namba kulingana na jedwali hapa chini.*
2. *Sasa pindua miraba hii tena - itaonekana hivi.*

   *Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.*

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

- Njia gani ilikuwa rahisi zaidi? Pamoja na maelekezo au la?
- Kwa nini ilikuwa rahisi mara ya pili?
- Pia tunapewa maelekezo ya jinsi tunavyopaswa kuishi. Je, tuna kitabu gani cha maagizo cha jinsi tunavyopaswa kuishi?
    - *Biblia*

Mungu alituumba na anatujua vizuri. Anajua kilicho bora kwetu na anatupenda. Anatutakia mema. Ili kutusaidia kufanikiwa maishani, anatupatia kitabu chenye maelekezo ya maisha. Tunapaswa kutii yale yaliyoandikwa humo. Hii haimaanishi kwamba hatutawahi kukutana na tatizo lolote. Biblia inasema kwamba kila mtu atakabili matatizo. Inamaanisha kuwa hata tunapokabili matatizo, Mungu hutusaidia kuyashinda.

## Kukua Kama Mungu Anavyokusudia

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO** (MW)

Katika Moduli ya 1, tulizungumzia maeneo 4 tunayopaswa kukua. Hayo maeneo 4 ni yapi?

- *Kiakili, Kiroho, Kimwili, Kijamii*

Ili kusaidia kuendeleza maeneo haya manne tunahitaji kuelewa kile ambacho Biblia - kitabu chetu cha maelekezo - kinasema badala ya kile utamaduni wetu unachosema.

Katika vikundi vidogo, jaza jedwali la Utamaduni Wetu na Biblia *(****VIONYESHI****).*

*Kwa kila jambo, fikiria juu ya kile ambacho kidesturi kinafanywa kanisani au katika utamaduni wako. Kisha soma mistari ya Biblia na uandike jambo kuu. Fikiria kama kanisa lako au desturi za kitamaduni ni sawa na kile Biblia inasema.*

***Maelekezo ya Mwezeshaji****: Iwapo una muda mchache, liambie kila kundi lifanye mada tofauti kwenye jedwali na kisha shirikisha majibu yao na kundi kubwa.*

| | UTAMADUNI WETU | BIBLIA |
|---|---|---|
| ***Kiakili*** | | |
| *Hekima* | | *Mithali 3:13-15* |
| ***Kijamii*** | | |
| *Ndoa* | | *Waefeso 5:33* |
| *Familia* | | *Waefeso 6:1-4; Mithali 22:6* |
| *Kuwapenda Wengine* | | *1 Yohana 3:16-17* |
| *Kuwapenda maadui* | | *Mathayo 5:43* |
| | **UTAMADUNI WETU** | **BIBLIA** |
| ***Kiroho*** | | |
| *Jinsi ya kuwa karibu na Mungu* | | *Mathayo 22:35-38* |
| *Uinjilisti* | | *Mathayo 28:18-20* |
| ***Kimwili*** | | |
| *Kujali Afya* | | *1 Wakorintho 6:19-20* |
| *Jinsi ya Kutunza/kusimamia fedha* | | *1 Timotheo 6:10; Mithali 21:20; 1 Timotheo 5:8; Waefeso 4:24* |
| *Kazi* | | *Wakolosai 3:23* |
| *Kuhifadhi mazingira* | | *2 Wathesalonike 3:10-12* |

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Mathayo 6:33

- Inamaanisha nini kuutafuta Ufalme wa Mungu?

Kama tulivyojifunza, Ufalme wa Mungu unaonekana popote tunapoona watu wakiishi kwa kutii mapenzi ya Mungu na kumheshimu akiwa Mfalme wa maisha yao. Hilo linamaanisha kwamba 'kuutafuta' Ufalme kunamaanisha kumtii Mungu zaidi. Haimaanishi kwamba tuombe tu. Tunahitaji kujitahidi kuwa watiifu zaidi kwa Mungu katika maeneo/nyanja zote za maisha.

**TAFAKARI BINAFSI**

Sasa chagua mada 1-2 kutoka kwenye Utamaduni Wetu na Biblia ambazo ungependa kuboresha maishani mwako na kuwa mwaminifu zaidi kwa maagizo ya Biblia. Andika mstari wa Biblia kutoka kwenye mada hizi katika kadi tupu na uzibandike mahali fulani katika nyumba yako ili uweze kuziona mara kwa mara wiki hii.

***Maelekezo ya Mwezeshaji**: Baada ya kila mtu kuandika mistari yake ya Biblia kwenye kadi, ombea wanakikundi ili waweze kukua katika kutii maagizo ya Mungu kwa maisha yao.*

# Somo la 5: Tumaini la Wakati Ujao

**Mawazo Makuu**

1. Ulimwengu ulivunjika wanadamu walipotenda dhambi, lakini Yesu alikuja kupatanisha vitu vyote.
2. Hakuna kilicho kikamilifu katika ulimwengu huu, lakini kwa kutembea kwa utii wa Mungu tunaweza kuanza kuona mabadiliko.

**Nyenzo**

1. Vionyeshi: Mabango ya Uhusiano (picha 4, pia zilitumika katika Moduli ya 1)
2. Mwongozo wa Mwanafunzi Hiari (MW): Jinsi ya kuwa Mjenzi wa Ufalme

## Injili Nzima

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Katika somo la kwanza katika Moduli ya 1, tuliuliza swali - "Kwa nini Yesu alikufa Msalabani?" Je, kuna mtu yeyote anayekumbuka jibu la swali hili?

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Sikiliza majibu yao kwa kifupi kisha onyesha na urudie kila picha kati ya hizo 4 (**VIONYESHI: Mabango ya Uhusiano**). Elezea kila bango::*

| | |
|---|---|
| Picture 1: Creation  | **Uumbaji** – Mungu alipoumba ulimwengu kila kitu kilikuwa kamilifu. |
| Picture 2: The Fall  | **Anguko** – Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, dhambi iliathiri sehemu zote za maisha.<br>● *Mwanadamu na Mwanadamu: Adamu na Hawa walianza kugombana na kulaumu.*<br>● *Mwanadamu na Mungu: Mungu hakutembea tena katika bustani pamoja na wanadamu kama hapo awali.*<br>● *Mwanadamu na Asili: Kazi ikawa ngumu, kuzaa kukawa kuchungu.* |

| | |
|---|---|
| Picture 3: Restoration  | **Msalaba** – Yesu alikuja kupatanisha vitu vyote (Wakolosai 1:20). |
| Picture 4: The Return  | **Kurudi** –Ulimwengu utakuwa mkamilifu tena baada ya Kristo kuja (Ufunuo 22). |

Sasa tuko kati ya picha 3 na 4. Kila kitu bado hakijakamilika. Baadhi ya ishara zipi zinazoonyesha kwamba ulimwengu bado haujakamilika?

## Kupatanisha Vitu Vyote

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Kifo cha Yesu kilianza upatanisho wa vitu vyote na Mungu alitukabidhi kazi ya kuendeleza kazi ambayo ameianza.

Soma 2 Wakorintho 5:17-20.

- Mungu alitupa huduma gani tuifanye?
    - *Huduma ya upatanisho*

Soma Wakolosai 1:20.

- Yesu alikuja kupatanisha?
    - *Vitu vyote*

Yesu Kristo alianza kazi kupitia kifo na ufufuko wake, na tumepewa kazi ya kuendeleza kile ambacho amekianza. Tunahitaji kuwa wawakilishi wake ili kuleta upatanisho.

- Tunawezaje kuwa wale wanaoleta upatanisho?

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Soma hadithi zifuatazo na jadili maswali baada ya kila hadithi.*

## Hadithi ya 1 - Usingizi Mzuri wa Usiku

Katika jumuia moja, wanawake wengi walikuwa wakiamka saa 7:00 usiku ili kuanza shughuli zao za kila siku. Kabla ya kifungua kinywa, walikusanya kuni, kuchota maji, na kuandaa chakula kwa ajili ya familia zao. Baada ya kifungua kinywa, wangefanya kazi kwa masaa mengi shambani na kushughulikia kazi nyingine za nyumbani. Kila jioni, wanawake walirudi nyumbani kwao wakiwa wamechoka kutokana na kazi za kutwa nzima, wakiwa na nguvu kidogo ya kupumzika na kufurahia wakati pamoja na familia zao.

Baada ya kuhudhuria mafunzo ya ndoa na familia ya TCT, viongozi wachache wa kanisa waliamua kutaka kuanza kuonyesha upendo kwa wake zao kwa kuwahudumia. Ingawa mwanzoni waliaibishwa na wazo hilo, wanaume hao walitaka kumtii Mungu katika sehemu zote za maisha yao, ikiwamo kuwahudumia wake zao. Baada ya mijadala mingi, waliamua kuamka kabla ya mtu mwingine yeyote ili kuepuka aibu ya wengine kujua wanawasaidia wake zao. Wanaume hao waliamka na wake zao saa 10 mapema asubuhi ili kusaidia maandalizi ya siku hiyo, wakiwaruhusu wake zao masaa tatu ya ziada ya kulala. Matokeo yalikuwa ya kushangaza! Wanawake, walihisi wamepumzika zaidi na kuthaminiwa na waume zao, waliweza kuweka muda na nguvu zaidi katika familia zao. Hii, kwa upande mwingine, ilitengeneza kaya zenye furaha na amani zaidi. Wanafamilia walianza kutumia muda mwingi pamoja na familia zikawa na nguvu na afya njema.

Jamii kwa haraka iligundua kuwa kuna kitu kimebadilika katika familia hizi, na wakaanza kuchunguza. Haikuwachukua muda mrefu kujua wanaume hao walikuwa wameamka saa 10 mapema asubuhi, wakiwaruhusu wake zao kulala zaidi. Badala ya kuwacheka wanaume, nao walianza kubadilika! Sasa, jua linapochomoza saa 10 asubuhi, pia familia hizo katika jumuia hiyo, zikichochewa na wanaume wachache wa kanisa waliotamani kuwahudumia wake zao. Familia katika jamii sasa zina furaha na afya njema zaidi. Inashangaza jinsi usingizi wa ziada unaweza kufanya!

- Kilitokea nini katika hadithi hii?
- Ni nini kilianzisha yote?
- Matokeo yalikuwa yapi?
- Je, sasa jumuia hii imefanya zaidi au kidogo kama vile Mungu anavyokusudia?
- Tunaweza kujifunza nini kutokana na hadithi hii?

## Hadithi ya 2 - Kutoka Kuteswa Hadi Kuongoza

Kulikuwa na mchungaji katika nchi nyingine iliyofungwa ambaye kila mara alikuwa akiitwa kituo cha polisi. Angalau mara sita kwa mwaka polisi walikuja kwenye mafunzo aliyokuwa akiendesha na kumpeleka kituo cha polisi. Siku moja alijifunza juu ya wazo la kujenga Ufalme wa Mungu na akaanza kufundisha kanisa lake mawazo hayo. Alilitia moyo kanisa lake na wale aliohusika nao kuanza kuwahudumia majirani zao na kutafuta fursa za kuifanya jumuia yao iwe zaidi kama Mungu alivyokusudia iwe.

Makanisa yalifanya miradi mingi: kuwapa wahitaji, kuwajengea wajane nyumba, kutengeneza barabara, kujenga vyoo n.k. Kanisa lilianza kukua na waumini wakakomaa zaidi. Uovu wa kijamii kama vile unywaji pombe na kamari ulikoma katika jumuia hii. Polepole maafisa wa serikali waliona matokeo chanya ambayo mchungaji huyu na makanisa aliyohusika nayo walikuwa nayo kwa jamii. Matokeo yake wakamfanya mchungaji huyo kuwa kiongozi mpya wa serikali ya eneo hilo. Alianza katika jukumu lake jipya kwa kufundisha wale walio chini yake masomo ya afya hivyo waliweza kumfundisha kila mtu katika jamii masomo haya. Sasa afya za wale wanaoishi katika jamii inaboreka.

- Mchungaji huyo alifanya nini?
- Anajenga Ufalme wa Mungu katika njia zipi?
- Matokeo yamekuwa yapi?
- Baadhi ya masomo gani kutoka hadithi hii tunayoweza kuyatumia katika maisha yetu wenyewe?

### Hadithi ya 3 - Watoto Wanaohudhuria Shuleni

Katika eneo moja idadi ya watoto waliohudhuria shule ilikuwa ndogo sana. Mtu mmoja, kwa kutambua umuhimu wa elimu, aliamua kujaribu kufanya kitu kuhusu hilo. Alizungumza na wengine kanisani kuhusu tatizo hilo na akakusanya timu ndogo ya watu waliokuwa tayari kufanya kazi naye kutatua tatizo hilo. Walianza kwenda nyumba kwa nyumba kuhimiza familia kupeleka watoto wao shuleni. Matokeo yake watoto wote katika eneo lake walikaa shuleni. Maafisa wa elimu katika maeneo mengine waliona kilichokuwa kikiendelea katika jamii yake na wakamkaribisha kwenda katika maeneo mengine kuwahimiza wazazi kuwaweka watoto wao shuleni. Sasa, sio tu watoto katika kijiji chake lakini pia katika vijiji vinavyozunguka wanakaa shuleni.

- Mtu huyo anajenga Ufalme wa Mungu katika njia gani?
- Inawezekanaje kufanya jambo kama hilo katika jumuia yetu?

Sote tunaweza kuwa mtu anayeleta mabadiliko katika jamii zetu. Watu hawa hawakuwa maalum au waliobarikiwa zaidi. Walikuwa watu wa kawaida kama mimi na wewe. Wengine walikuwa na elimu ndogo sana lakini wote walikuwa tayari kufanya yote wawezayo ili kujenga Ufalme wa Mungu katika jumuia yao.

## Jinsi ya kuwa Mjenzi wa Ufalme

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO** (MW)

Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka. Angeweza kujenga Ufalme wake bila sisi. Lakini huo sio mpango wake; Mpango wake ni kututumia katika kuujenga Ufalme wake. Kujenga Ufalme wa Mungu huanza na sisi.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Soma jinsi ya kuwa Mjenzi wa Ufalme. Waombe wanafunzi kufikiria kwa maombi juu ya jinsi wanavyoweza kuwa Wajenzi wa Ufalme.*

### 1. Anza na wewe mwenyewe

Hatua ya kwanza ya kuona Ufalme wa Mungu ukijengwa katika maisha yako, katika familia yako, katika kanisa lako, katika jumuia yako, na ulimwenguni ni kujichunguza mwenyewe. Je, uko tayari kutumiwa na Mungu? Je, uko tayari kuwa mtiifu kwa Mungu katika kila eneo la maisha yako? Ni jambo gani moja au mawili unaweza kufanyia kazi kujiboresha wiki hii?

### 2. Fundisha na uitie moyo familia yako

Unapoanza kutumia Ufalme wa Mungu katika kila sehemu ya maisha yako unahitaji kuanza kuitia moyo familia yako kufanya vivyo hivyo. Tunaposoma, tunapaswa tuwe tunafundisha familia zetu kila wakati (Kum. 6:7) haijalishi tunafanya nini. Tafuta njia za kufundisha familia yako kwa kile unachofanya, kwa kuzungumza nao, na kwa kutafuta njia za kuwasaidia kuanza kuwatumikia wengine pia.

Kumbuka mambo uliyojitolea kufanya kwenye somo katika kila moja ya maeneo manne ili pia kuisaidia familia yako kukua.

### 3. Mwombe Mungu akutumie kuwabadilisha wengine

Anza kuomba na kumwomba Mungu akusaidie kuwabadilisha wengine. Tafuta fursa. Unapowaona watu wana uhitaji, mwombe Mungu akuonyeshe jinsi unavyoweza kuwasaidia watu hao.

Mungu yuko tayari zaidi kutusaidia kujenga Ufalme wake. Atatufunulia kwa wakati unaofaa, njia sahihi ya kusaidia.

### 4. Watumikie Wengine

Shiriki katika Matendo ya Upendo na utafute njia zingine za kuhudumia. Hata kama unahisi kuwa huna uwezo wa kufanya mengi, bado unapaswa kutumia talanta zote ambazo Mungu amekupa kutumikia. Unapohudumu, utaanza kukua na utapata uwezo wa kufanya zaidi na zaidi.

# Somo la 6: Tumia Kila Kitu Mungu Alichokupa

**Mawazo Makuu**

1. Mungu ametupa mengi sana, na anatarajia tutumie kila kitu tulicho nacho kwa ajili ya ufalme wake.
2. Tunahitaji kutumia talanta zetu, hazina, na pesa kwa kusudi lake. Tunapofanya hivyo, Mungu anaweza kulizidisha ili kutimiza jambo kubwa zaidi.

**Nyenzo:**

1. Vionyeshi:
    a. 6.1 Igizo Mfano la Talanta (nakala 5)
    b. 6.2 Igizo la Daudi na Goliathi (nakala 5)
2. Karatasi ya Bango

## Hadithi 3 za Biblia

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Kabla ya somo kuanza waombe watu 10 wa kujitolea kutayarisha na kuigiza igizo maigizo mawili (**Vionyeshi**). Hapa kuna maigizo mawili na utahitaji watu wangapi wa kujitolea kwa kila moja:*

- *6.1 Mfano wa Talanta (Mathayo 25:14-30) - 5 Wakujitolea*
- *6.2 Daudi na Goliathi (1 Samweli 17:12-54) - 5 Wakujitolea*

### Igizo la 1 - Mfano wa Talanta (Mathayo 25:14-30)

Mfano wa Talanta umetushtua kila wakati. Katika Biblia nzima tunaona moyo wa Mungu kwa maskini na jinsi anavyopinga udhalimu na uonevu. Lakini katika hadithi hii, kila mtu alipewa kiasi tofauti cha talanta. Kisha yule aliyepewa kidogo zaidi aliadhibiwa na kupoteza vyote alivyokuwa navyo! Tunahitaji kuutazama mfano huu kwa makini na kuuelewa.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Waombe watu 5 waliojitolea kuigiza igizo la Talanta. Kisha uliza maswali ya majadiliano na uhakikishe kuwa wanaelewa mambo mawili ya mwisho hapa chini.*

**Igizo la Mfano wa Talanta**

(Katika Mathayo 25:14-30)

***Bwana, Watu 5 wa Kujitolea - Mwalimu, Mtumishi 1, Mtumishi 2, Mtumishi 3, Msimulizi wa Hadithi***

**Bwana:** Watumishi, njooni hapa msikilize. Ninakaribia kwenda safari ya kikazi. Hapa kuna talanta tano ninawapa mzitunze ( *mpe talanta tano Mtumishi wa 1).*
...talanta mbili kwa ajili yako ( *mpe talanta mbili Mtumishi wa 2*)...
....na hapa kuna talanta 1 kwako ( *mpe talanta moja mtumishi wa tatu*).
Kwaheri.

**Mtumishi wa 1:** Aisee, pesa nyingi sana. Lazima nizitumie kwa busara *(anaondoka).*

**Mtumishi wa 2:** Ni bora nizitumie pesa hizi kwa busara. Bwana ana matarajio makubwa *(anaondoka).*

**Mtumishi wa 3:** Loh, kitatokea nini nikipoteza talanta hii - maisha yangu yataharibiwa! Ngoja, najua, nitaichimbia na kuficha ardhini. (*anaondoka*)

**Msimulizi wa hadithi***:* Baada ya muda mrefu, Bwana wa watumishi anarudi na kuwaita watumishi wake watoe hesabu.

**Mtumishi wa 1:** Bwana, ulinikabidhi talanta tano; hapa, nimepata talanta tano zaidi. *(Anarudisha talanta 10).*

**Bwana:** Umefanya vizuri mtumishi mwema na mwaminifu. Umekuwa mwaminifu kwa machache; nitakuweka juu ya mengi. Ingia katika furaha ya bwana wako.

**Mtumishi wa 2:** Bwana, ulinikabidhi talanta mbili; hapa, nimepata talanta mbili zaidi. *(Anarudisha talanta 4).*

**Bwana:** Umefanya vizuri mtumishi mwema na mwaminifu. Umekuwa mwaminifu kwa machache; nitakuweka juu ya mengi. Ingia katika furaha ya bwana wako.

**Mtumishi wa 3:** Bwana, nalijua ya kuwa wewe ni mtu mgumu, wavuna pale ambapo hukupanda, na kukusanya pale ambapo hukutawanya mbegu; basi niliogopa, nikaenda nikaificha talanta yako ardhini. Hapa, unayo iliyo yako. *(Anatoa talanta 1).*

**Bwana:** Wewe mtumishi mbaya na mvivu! Ulijua kwamba mimi huvuna mahali ambapo sikupanda na kukusanya ambapo sikutawanya? Basi, ingalikupasa kuiwekeza fedha yangu kwa watoa riba, nami nilipokuja ningepokea iliyo yangu pamoja na faida. Askari! Mnyang'anye talanta hiyo na mpe yule aliye na talanta kumi. Kwa maana kila aliye na kitu ataongezewa, naye atakuwa na tele. Lakini yule asiye na kitu, hata kile alicho nacho kitachukuliwa. Na mtupeni mtumwa asiyefaa katika giza la nje. Mahali hapo kutakuwa na kilio na kusaga meno.

**Maswali ya Majadiliano:**

- Kwa nini bwana anawapongeza wale walio na talanta tano na talanta mbili?
- Kwa nini bwana anamkemea mwenye talanta moja?
- Kinatokea nini kwa mtu aliye na talanta moja?
- Tunaweza kujifunza nini kutokana na mfano huu?
    - *Mungu anataka tutumie kile alichotupa bila kujali ni kikubwa au kidogo.*
    - *Tunapotumia kile ambacho Mungu ametupa, atazidisha.*

## Igizo la 2 – Daudi na Goliathi (1 Samueli 17:12-54)

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Waombe watu 5 waliojitolea kuigiza igizo la Daudi na Goliathi kwa kutumia* ***VIONYESHI****: Igizo la Daudi na Goliathi. Kisha uliza maswali ya majadiliano hapo chini.*

### Igizo la Daudi na Goliathi

(Katika 1 Samueli 17:1-54)

***Watu 5 wa kujitolea - Daudi, Ndugu, Askari, Sauli, Goliathi***

**Daudi**: Habari ndugu! Ninawaletea chakula ambacho baba yetu aliwaandalia. Hali ya mapigano ikoje?

**Ndugu**: Kuna jitu liitwalo Goliathi. Kila siku anakuja na kutupa changamoto lakini hakuna anayethubutu kupigana naye. Yeye ni mkubwa sana! Mfalme alisema kwamba atatoa zawadi kubwa kwa yule atakayemuua.

**Daudi**: Ni nani huyu hata majeshi ya Mungu aliye hai yanamwogopa? Tunahitaji kupigana naye kwa sababu Mungu wetu atatusaidia!

**Ndugu**: (*Kwa hasira*) Wewe ni nani wa kusema hivyo? Wewe ni mvulana tu anayechunga kondoo, na unajiona kuwa wa maana.

**Askari**: Daudi, tembea njia hii. Tumesikia ulichosema kuhusu Goliathi na mfalme Sauli anataka kukuona.

**Daudi**: Mfalme anataka kuniona? Mimi ni mvulana tu.

*(Anaenda nje kukutana na Sauli)*

**Daudi**: (*Akizungumza na Sauli*) Tafadhali usikate tamaa kwa sababu ya Mfilisti huyu. nitakwenda kupigana naye.

**Sauli**: Huwezi kwenda kupigana naye. Wewe ni mdogo sana na amekuwa mtu wa vita tangu ujana wake.

**Daudi**: Mtumishi wako alikuwa akichunga kondoo kwa baba yake. Na alipokuja simba, au dubu, na kukamata kondoo katika kundi, nilimfuata, nikampiga, na kumwokoa kinywani mwake. Naye akiniinuka, nilimshika ndevu zake, nikampiga na kumuua. Mtumishi wako amewaua simba na dubu wote wawili, na huyu Mfilisti asiyetahiriwa atakuwa kama mmoja wao, kwa kuwa ameyatukana majeshi ya Mungu aliye hai. Bwana aliyeniokoa na makucha ya simba na makucha ya dubu ataniokoa na mkono wa Mfilisti huyu.

**Sauli**: Nenda, na Bwana awe pamoja nawe. Hii hapa silaha yangu, ivae.

**Daudi**: *(Jifanye umevaa silaha na kutembea kwa shida kidogo.)* Silaha hii ni kubwa sana, siwezi kuivaa kwa sababu sijaizoea. *(Jifanye unavua silaha na kuokota mawe matano madogo chini. Nenda nje, upigane na Goliathi.)*

**Ndugu**: Ni nini kinaendelea hapa? Angalia, kijana anafanya nini? Ni mjinga kweli. Familia yetu itaaibishwa kwa sababu yake!

**Goliathi**: (*Anamtazama Daudi*) Je, mimi ni mbwa kwamba unanijia na fimbo? Njoo kwangu, nami nitawapa ndege wa angani na wanyama wa mwitu nyama yako.

**Daudi**: Wewe unanijia mimi na upanga na mkuki, lakini mimi nakujia wewe kwa jina la Mwenyezi-Mungu wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli uliyemtukana. Leo hii Bwana atakutia mkononi mwangu, nami nitakupiga na kukukata kichwa. Nami leo nitawapa ndege wa angani na wanyama wa mwitu mizoga ya jeshi la Wafilisti, ili dunia yote ipate kujua ya kuwa yuko Mungu katika Israeli, na kwamba kusanyiko hili lote lipate kujua ya kuwa Bwana haokoi kwa upanga wala kwa mkuki. Kwa maana vita ni vya Bwana, naye atawatia ninyi mikononi mwetu.

**Goliathi:** *(anamkaribia Daudi na kujiandaa kushambulia.)*

**Daudi:** *(anajifanya kuzungusha kombeo na kulirusha kuelekea kwa Goliathi)*

**Goliathi:** *(anajifanya kupigwa na kuanguka na kufa)*

**Daudi:** *(anamkimbilia na kukata kichwa cha Goliathi.)*

**Sauli, Ndugu na Askari:** *(Wakishangilia)* Mungu anatupa uhuru!

**Maswali ya Majadiliano:**

- Je, Daudi alikuwa tajiri, mwenye kipawa au maarufu?
    - *Hapana, Daudi alikuwa kijana tu. Alikuwa na ujuzi fulani aliojifunza kutokana na kuchunga kondoo, lakini alitegemea hasa msaada kutoka kwa Mungu.*
- Daudi alifanya nini ili kushinda dhidi ya Goliathi?
    - *Alitumia talanta alizokuwa nazo. Uwezo wake ulikuwa rahisi kwa sababu alikuwa bado kijana, lakini bado alikuwa tayari kuutumia kwa kusudi la Mungu.*

- Matokeo yalikuwa yapi?
    - *Mungu alitukuzwa na taifa likawa huru*.

## Hadithi – Mjane na Nabii Eliya (1 Wafalme 17)

Soma 1 Wafalme 17:8-16.

- Mjane alikuwa na nini?
- Nabii Eliya alimwomba nini?
- Matokeo yalikuwa yapi?
- Unafikiri ni kwa nini Mungu alimtuma nabii Eliya kwa mjane huyu? Kulikuwa na Waisraeli wengi walioishi huko, na si wote wangekuwa maskini kama mjane huyo.
- Kwa nini Mungu alimbariki mjane kabla hajatoa?

# Mungu Huzidisha

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO**

Katika kila igizo tunatambua somo muhimu. Kila mmoja alitumia chochote alichokuwa nacho kama Mungu alivyowapa. Daudi hakuwa na pesa, lakini alitumia ujuzi aliojifunza. Mjane pia hakuwa na pesa, lakini alitumia mlo wake wa mwisho. Ni pale tu walipokuwa tayari kutumia walicho nacho, ndipo Mungu alipokizidisha na kufanya kazi kwa njia za ajabu.

Mungu ametupa nini? Ni rahisi kuamini katika uwongo kwamba hatuna chochote, lakini hii si kweli.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Hapa chini kuna aina 4 za rasilimali ambazo Mungu ametupa ili tuzitumie. Panga aina moja kwa kila kikundi. Waambie watengeneze orodha kwenye karatasi ya mifano 10-20 ya aina hiyo ya rasilimali. Kisha kila kikundi kiwasilishe karatasi/bango lao kwenye kundi kubwa.*

*Mifano michache imetolewa. Tumia mifano ili kuhakikisha kuwa kila kikundi kinaelewa aina ya rasilimali, kisha waache watoe mifano yao wenyewe 10-20.*

- Rasilimali za Kiroho - *maombi, upendo wa Mungu, hekima ya Mungu*
- Uwezo – *uwezo wa kupika, uwezo wa kulima, uwezo wa kujenga nyumba*
- Maarifa - *maarifa ya afya, maarifa ya ujuzi mzuri wa malezi*
- Rasilimali za Kimwili – *nyumba, mavazi, miili yenye afya na nguvu, chakula*

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Angalia mabango yote ya rasilimali na ujadili:

- Ni rasilimali gani tulizo nazo tunazohitaji kutumia zaidi kwa ajili ya Mungu?
- Kama kanisa, tunawezaje kutumia vitu hivi kumtumikia Mungu?
- Ni jambo gani moja unaweza kufanya mwezi huu ili kutumia vyema rasilimali uliyo nayo kwa ajili ya Mungu?

# Somo la 7: Fanya Kazi Ili Kumtukuza Mungu

**Mawazo Makuu**

1. Tunamtukuza Mungu tunapofanya kazi kwa bidii.
2. Tumeitwa kuwa mawakili wa uumbaji wa Mungu.

**Nyenzo**

Karatasi ya Bango

## Kwa Nini Tufanye Kazi??

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO**

- Baadhi ya sababu za kufanya kazi ni zipi? Tumia mistari ifuatayo na mawazo yoyote uliyo nayo hadi sasa katika somo hili.
    - 1 Wathesalonike 4:11-12
    - 1 Timotheo 5:8
    - Waefeso 4:28
    - 1 Wakorintho 10:31

**TOA RIPOTI**

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

- Je, unafikiri Mungu anakusudia tufanye kazi?
- Watu huwa na mtazamo gani kuhusu kazi?
- Mungu alipokuwa anapanda bustani (Mwa 2:8), au Yesu alikuwa seremala (Marko 6:3), unafikiri mtazamo wake ulikuwaje kuhusu kazi?
- Tunawezaje kuwa na mtazamo zaidi kama Mungu?
- Tunaweza kuwasaidiaje wengine wawe na mtazamo kama wa Mungu juu ya kazi yao?

## Mungu Anajali Jinsi Tunavyofanya Kazi Zetu

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Mara nyingi imesemwa kwamba wafanyikazi wa Kikristo ndio wafanyikazi wabaya zaidi.

- Kwa nini unafikiri hiyo itakuwa kweli?
- Je, hutokea katika eneo lako?
- Unafikiri Mungu anahisije kuhusu Wakristo kuwa na sifa hii?

Ingawa Biblia haipendekezi kamwe kazi fulani ni muhimu zaidi au zisizo muhimu, Biblia ina mengi ya kusema namna tunavyopaswa kufanya kazi zetu. Ni sehemu muhimu ya siku zetu—tunatumia muda mwingi wa kuamka kufanya kazi, hivyo tunahitaji kufikiria kwa makini jinsi tunavyofanya kazi yetu.

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO**

Angalia mistari ifuatayo katika vikundi vidogo. Mistari hii inatufundisha nini kuhusu kazi? Fupisha aya zote nne katika sentensi moja.

- 2 Wathesalonike 3:10-12
- Mithali 10:4
- Mithali 19:15
- Mithali 21:25

**TOA RIPOTI**

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Unafikiri mistari hii inafundisha nini kuhusu tunavyopaswa kufanya kazi?

- 1 Wakorintho 10:31 - *Mtukuzeni Mungu*
- Wakolosai 3:23- *Fanya kazi kana kwamba unamtumikia Mungu*

Muda mwingi wa maisha ya Yesu alikuwa seremala. Hebu fikiria ungeweza kumwona kama seremala.

- Unafikiri ubora wa kazi yake ulikuwaje?
- Fikiria ulifanya kazi naye katika warsha/karakana: ingekuwaje kufanya kazi katika warsha ileile na Yesu?
- Angefanyaje wakati wa mchana?
- Angefanyaje wakati ambapo hakuna mtu aliyekuwa anamtazama?

## Kilimo cha Kumtukuza Mungu

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Wengi wetu tuna uzoefu wa kufanya kazi kama wakulima. Soma Mwanzo 1:28-29 na 2:15. Haya ndiyo maagizo ya kwanza kabisa ambayo Mungu alimpa mwanadamu.

- Mungu anasema tufanye nini katika mistari hii?

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Kutoka vifungu viwili vya Biblia, hakikisha kwamba kikundi kinaona maagizo makuu matatu - lazima tufanye kazi, tutunze, na tutawale uumbaji.*

Hata kabla ya mwanadamu kutenda dhambi, Mungu anatupangia tuutunze uumbaji. Hata hivyo, kwa sababu ya Anguko kazi yetu ikawa ngumu zaidi. Lakini ingawa kazi ni ngumu zaidi sasa, bado ni kile ambacho Mungu ametuomba tufanye.

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO**

Katika mistari ambayo tumesoma hivi punde, Mungu alitupa maagizo matatu: fanya kazi, tunza, na utawale uumbaji.

- Fanya Kazi = Hii ina maana kwamba tunahitaji kuendeleza uumbaji ili uweze kuzalisha zaidi. Tunapotumia mbinu bora za kilimo tunafanya kazi ya uumbaji.

- Tunza = Hii ina maana tunahitaji kulinda uumbaji na sio kuudhuru. Tunapotumia mbolea nyingi au dawa za wadudu tunaweza kudhuru uumbaji. Kuzuia mmomonyoko wa udongo na kukomesha uchafuzi wa mazingira pia ni njia za kulinda uumbaji.

- Tawala = Hii ina maana tuna mamlaka juu ya uumbaji. Ikiwa wadudu au panya wanasababisha matatizo, tunahitaji kuwakomesha (kama walivyofanya Wahindi wa Pokomchi ambao tulijifunza kuwahusu katika Somo la 2 la Moduli ya 3). Kutawala juu ya uumbaji pia kunamaanisha tunaweza kupata suluhu za kujilinda na majanga ya asili, na wakati mwingine hata kuyazuia.

Katika vikundi vidogo::

1. Toa mada moja kwa kila kikundi - fanya kazi, tunza, na tawala uumbaji. Waambie watengeneze orodha kwenye karatasi ya bango ya njia mahususi wanazoweza kufanya hivyo katika jumuia yao. Kisha kila kikundi kiwasilishe bango lao kwenye kundi kubwa.
2. Vikundi vyote vinapomaliza kuwasilisha mabango yao, liambie kundi kubwa libainishe ni mambo gani kutoka kwenye orodha yanaweza kufanywa kama Tendo la Upendo na kanisa. Wekea nyota.

**TAFAKARI BINAFSI**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Soma maswali yafuatayo na utulie kwa dakika 1 baada ya kila swali ili washiriki wape muda wa kutafakari kwa utulivu.*

- Je, unafanya kazi, unatunza na kutawala uumbaji kama Mungu alivyokusudia?
- Je, unafikiri Mungu anafurahishwa na jinsi unavyofanya kazi?
- Baadhi ya mambo gani unaweza kuyabadilisha wiki hii?

# Somo la 8: Ukweli Kuhusu Shetani

**Mawazo Makuu**

1. Tunahitaji kutambua njia ambazo Shetani hujaribu kutudanganya.

**Nyenzo**

1. Vionyeshi: Mabango ya Uongo wa Shetani (seti moja ya mabango 8 kutoka kwenye Moduli ya 3)

## Shetani ni Mwongo

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Yohana 8:44.

Shetani ni mwongo. Anatudanganya ili kutuweka katika umaskini daima.

- Baadhi ya uwongo wa Shetani ni upi? Je, unakumbuka uwongo wowote ambao tumezungumza juu yake hapo awali?

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Pitia uwongo huu nane ukitumia mabango (**VIONYESHI**) na jedwali lililo hapo chini. Kwa kila uwongo, waambie wanakikundi wabainishe mambo mawili:*

*1) Matokeo ya uwongo huu ni yapi?*
*2) Ukweli ni upi?*
- *(Tumia jedwali lililo hapo chini hakikisha kuwa wanaelewa ukweli ukilinganisha na kila uwongo.)*

*Njia nyingine, unaweza kuwaomba watu 8 wa kujitolea kushikilia bango la kila uwongo, soma uongo huo kwa sauti, kisha uliza maswali mawili kwa kikundi. Sikiliza kuhakikisha kikundi kinaelewa ukweli wa Mungu katika kujibu.*

| UONGO WA SHETANI | UKWELI WA MUNGU |
|---|---|
| Kazi ni laana na mzigo mzito. Ni vizuri kufanya kazi kidogo iwezekanavyo. | Tumeumbwa kufanya kazi. Adamu alifanya kazi kabla ya anguko. Ni sehemu ya hadhi yetu na njia tunayoweza kumtukuza Mungu. |
| Tulizaliwa maskini na tutakufa maskini. | Mungu atatubariki ikiwa tutakuwa watiifu kwake. |

| | |
|---|---|
| Sisi ni maskini sana hatupaswi kutoa. Watu wengine wanapaswa kutupa.<br> | Hata walio maskini kabisa hawana sababu ya kutotoa. Katika Malaki Mungu anawaambia watu kwamba hawajabarikiwa kwa sababu hawamtangulizi Mungu. Anawaambia wamjaribu na kuona kitakachotokea wakianza kutoa kama alivyoamuru. Tunapaswa kutoa tukitambua kwamba Mungu ametupa kila kitu na yuko tayari kutupatia yote tunayohitaji. |
| Mungu anajali tu mambo ya kiroho.<br>  | Mungu anajali nyanja zote za maisha yetu. Vitu vyote vilivunjika katika anguko na anataka kupatanisha kila kipengele cha maisha yetu kumrudia yeye. |
| Mungu anataka tu tuwahubirie jirani zetu—hatuhitaji kushughulikia mahitaji yao ya kimwili.<br> | Mungu ametuambia tuwapende jirani zetu. Anapofafanua kondoo na mbuzi anatukumbusha kwamba upendo ni kutoa chakula, maji na makao. Alipoulizwa jirani yetu ni nani, Yesu alisimulia kisa cha Msamaria aliyekutana na mgeni aliyekuwa amejeruhiwa barabarani na kumpatia msaada wa matibabu. |
| Hatuwezi kubadilisha maisha yetu bila fedha kutoka kwa mtu mwingine.<br> | Mungu ameshatubariki. Tunahitaji kufungua macho yetu na kuona yote ambayo Mungu ameshatupa na kuanza kutumia hayo. Tunapotumia kile ambacho Mungu ametupa na kuwabariki wengine ndipo atatubariki. Katika Awamu ya 1 tulizungumza kuhusu Bi. Lee aliyewasaidia watu kwa kuwaletea mawazo tu. |

| | |
|---|---|
| Watu wengine ni bora kuliko watu wengine. Sisi sio muhimu.<br> | Sisi sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu na Mungu anampenda kila mmoja wetu hata akamtuma mwanae afe kwa ajili yetu. Hakuna watu wa juu na wa chini katika ufalme wake. Amemuumba kila mmoja wetu kulingana na jinsi anavyotutaka na ana kusudi maalum kwa kila mtu. |
| Ujumbe wa injili hubadilisha maisha yetu ya kiroho pekee.<br> | Yesu alikufa ili kupatanisha sehemu zote za maisha, si mambo ya kiroho tu. |

## Kweli ya Mungu Itatuweka Huru

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Yohana 8:32

- Kitakachotuweka huru ni kipi?

Sikiliza hadithi zifuatazo na ufikirie jinsi Mungu alivyowasaidia watu hawa kubadili maisha yao.

**<u>Hadithi ya 1</u>**

Baada ya dhoruba kubwa mnamo 2009, daraja la kusimamishwa, lililokuwa muhimu sana katika eneo hilo, lilisombwa na maji. Hili lilikuwa daraja muhimu kwa sababu lilisaidia watu katika jumuia za pande zote za daraja hilo kusafiri, kwenda na kurudi na bidhaa za biashara. Daraja hilo liliposombwa, msongamano katika eneo hili ulikuwa umesimama na jamii ilitengwa. Hapo mwanzo, Kamati ya Huduma Kubwa ya kanisa ilifikiri walikuwa maskini sana kuweza kujenga upya daraja. Hata hivyo, kwa sababu tatizo hili liliathiri maeneo mengi ya maisha - maeneo ya kitamaduni, kiuchumi na kijamii - walikusanyika pamoja wakaomba na kuliita kanisa zima kujadili mipango ya kutatua tatizo. Wote walikubali kushiriki katika kazi hii mara moja. Mmoja alikata miti kutengeneza marundo ya daraja, mwingine mbao na wengine wengi walitoa fedha kununua vifaa vya ujenzi kama vile saruji, mawe na mchanga. Kila mtu kanisani alishiriki katika kazi hii. Baada ya siku tatu, walikamilisha daraja la muda. Wanafunzi waliweza kwenda shuleni tena na biashara inaweza kuendelea.

Miezi mitano baadaye, daraja hili la muda mfupi lilianza kuvunjika na watu hawakuweza kupita. Kukabiliana na tatizo hili kubwa, kamati ya kanisa iliendelea kuomba na kuliita kanisa zima kuwa na umoja kutatua tatizo hilo. Mwanzoni, likikabili uhitaji huu mkubwa, kanisa lilifikiri kwamba wasingeweza kufanya lolote. Walifikiri kutatua tatizo hilo kubwa lilikuwa nje ya uwezo wao. Hivyo, baada ya kusali, kamati iliamua kuwasilisha tatizo hili kwa mkuu wa kijiji ili aweze kuhamasisha jamii kuchangia na kushirikiana na kanisa katika kutatua tatizo hilo.

Asante Mungu wetu! Daraja lilijengwa upya, na watu waliweza kupita kwa usalama tena. Jamii nzima ilifurahi kwamba waliweza kutimiza jambo walilodhani haliwezekani. Katika ujenzi wa daraja, mchango mkubwa ulikuwa kutoka kanisani. Serikali ya mtaa pia ilichangia chuma ili kuimarisha daraja. Sasa daraja linaweza kutumika kwa muda mrefu na jamii.

Daraja hilo lilikuwa na urefu wa mita 120 na upana wa mita 1.4. Ilichukua siku 15 kukamilisha. Kwa wastani, kulikuwa na vibarua 110 walioshiriki katika ujenzi kila siku - siku 1650 za kazi kwa jumla. Kila mtu alipojua hilo, walilipongeza kanisa. Ili kuwapongeza watu katika jamii na kuwatia moyo maeneo ya jirani, serikali ilitangaza jambo hilo katika magazeti na televisheni. Kupitia kazi hii, jina la Bwana Mungu wetu lilitukuzwa.

Kanisa lilipata heshima si tu kutoka kwa watu katika jamii, bali pia kutoka serikali ya mtaa. Maafisa hao mara kwa mara humtembelea mchungaji sasa ili kuomba msaada katika masuala ya umma. Vijana katika jamii walipokuwa wakisababisha matatizo, polisi walifika kwa mchungaji. Mchungaji aliwaambia hivi: “Acheni tu tuwe na uhuru wa kuwafundisha vijana, na ndipo mtakapoona mabadiliko.” Kwa kuona mifano ya mchungaji na familia yake, maafisa walisema kwamba wanatamani wanafunzi wangekuwa kama wao. Watu sasa mara nyingi wanaamini kwamba chochote ambacho serikali haiwezi kufanya, kanisa linaweza kulifanya.

- Baadhi ya uongo gani ambao kanisa hili liliushinda?
    - Kanisa ni duni/maskini sana, hawana uwezo
    - Hitaji ni kubwa sana, hatuwezi kufanya.

**Hadithi ya 2**

Mchungaji mmoja na mkufunzi wa TCT alitafakari juu ya mabadiliko yote aliyoyaona kijijini kwake wakati wa programu ya TCT. Alisema jambo la kwanza lililobadilika sana ni imani yao. "Kabla ya [kusoma TCT], watu wengi hawakuwa na wasiwasi kuhusu jamii na wengine. Wanakijiji na washiriki wa kanisa walifikiri tu kwamba jumuia ilihitaji mtu wa kuja (pengine kutoka Marekani) ili tuwe vizuri na kuendelea. Sasa kwa hakika tunajua Mungu ametufanya kuwa wahudumu wa upatanisho.” Ndani ya wilaya yao, kijiji cha mchungaji huyu kilikuwa kibaya zaidi. Watu walisema kijiji chao kilikuwa sehemu chafu zaidi, iliyojaa taka na samadi. Baada ya kusoma somo la 4 na kujifunza kwamba Mungu anajali kuhusu afya na usafi, kanisa lilihamasishwa kubadili hili. Kijiji kizima kina vyoo sasa--hata wengine wana mabomba ya maji. Pia walijenga uzio kuzunguka kijiji kizima, hivyo ng'ombe na nyati hawawezi kuingia na kutangatanga mitaani. Na vikundi vya wanawake hufanya kazi ya kusafisha kijiji Jumamosi ya kwanza ya kila mwezi. Sasa jumuia yao imeitwa Kijiji Safi Zaidi na NGO na serikali. Watu wana furaha mno; wanafurahia kuishi mahali pasafi. Sasa kanisa lilielekeza mawazo yao kwenye tatizo lingine: kwa sababu kijiji kiko maili 35 kutoka mji wa soko, watu walijitahidi kununua chakula cha kutosha. Kanisa lilipanga wafanyakazi wa kurekebisha barabara mbovu iliyounganisha kijiji chao na barabara kuu, ili kurahisisha usafiri. Kisha mchungaji akawa na wazo la kuanzisha soko lao wenyewe, ili watu wasilazimike kwenda hadi mji mkubwa kununua walichohitaji. Kanisa liliunda timu ya jumuia iliyomwendea kiongozi wa kijiji na wazo hili, na wakawaalika viongozi wote kuhudhuria ili kulijadili. Kijiji kiliwasaidia kuanza. Kwa hiyo sasa wananunua bidhaa kutoka mjini na kuzisafirisha hadi kijijini kuuza. Wanatumia faida kama hazina ya jamii kusaidia maskini zaidi na walio hatarini zaidi; hazina/mfuko huo unasimamiwa na kamati. Kila mara wanapouza bidhaa zote, wanawasilisha ripoti kwa viongozi wa kijiji. Sasa kanisa lina uhusiano mzuri na jamii, watu wanaweza kusafiri kwa urahisi zaidi na pia wana chakula cha kutosha, watoto wanaugua kidogo kwa sababu wanaishi katika mazingira safi, na watu wanafurahi kuishi katika kijiji chao, hawasubiri tena wengine waje kuwasaidia. Mungu asifiwe kwa mabadiliko haya!

- Ni uwongo gani ambao kijiji hiki kilikuwa kikiamini?
    - Tunahitaji tu kujijali wenyewe.
    - Sisi ni maskini sana hatuwezi kusaidia mtu mwingine.
    - Kanisa hushughulikia mambo ya kiroho pekee.

- Kilifanyika nini walipoelewa ukweli?

**TAFAKARI NA MWENZAKO**

Tumia dakika chache kutafakari juu ya wakati ambapo ulivunjika moyo au ulifikiri jambo fulani haliwezekani. Je, unafikiri haikuwezekana kweli, au ulikuwa mwathirika wa uwongo wa Shetani? Mshirikishe mwenzako.

Baada ya kushirikisha, fikiria njia ambazo unaweza kukumbuka kuamini katika ukweli wa Mungu wakati ujao jambo kama hilo linapotokea. Kumbuka kwamba Yesu anakuja kutuweka huru, lakini Shetani anataka kutuweka katika utumwa.

# Somo la 9: Kuwafunza Wengine

**Mawazo Makuu**

1. Sote tunaweza kuwafunza wengine na lazima tufanye hivyo.
2. Tunaweza kuwafunza wengine kwa kuwa mfano mzuri.

**Nyenzo**

Hakuna

## Agizo Kuu

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma Mathayo 28:19-20.

- Mungu anatuamuru tufanye nini?
    - Kufunza mataifa yote
    - Kuwabatiza
    - Kuwafundisha kutii kila kitu ambacho Yesu aliamuru.

Tumeagizwa kufanya wanafunzi; kuna sehemu mbili katika amri hii. Sehemu ya kwanza ni kuona watu wakiokolewa na kubatizwa. Tayari tulijadili jinsi ya kufanya hivi katika moduli ya mafunzo juu ya Uinjilisti. Sehemu ya pili ya amri ya Yesu ni kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

**MJADALA WA KIKUNDI KIDOGO**

Katika vikundi vidogo jadili maswali haya:

- Tunafanyaje wanafunzi katika Kanisa letu?
- Yesu alifanya mambo gani ili kufanya wanafunzi?
    - *Alitumia muda pamoja nao*
    - *Aliwafundisha*
    - *Aliwatia moyo na kuwapa changamoto*
    - *Aliwahudumia*
- Kuna tofauti gani kati ya jinsi tunavyofanya wanafunzi na jinsi Yesu alivyofanya wanafunzi?
- Nani anayeweza kufanya wanafunzi?
    - *Waumini wote, sio viongozi pekee.*

## Uwe Mfano Mzuri kwa Wengine

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Sehemu moja ya kufanya wanafunzi ni kwamba tunaishi maisha yetu kama mfano mzuri kwa wengine kuufuata.

Soma Wafilipi 3:17 na 1 Wakorintho 4:6 na 11:1.

- Maagizo ya Paulo katika mistari hii yalikuwa yapi?

Soma 2 Wathesalonike 3:6-9.

- Kwa nini Paulo aliamua kutopokea msaada wa kifedha?

Soma Tito 2:7-8.

Paulo alimshauri nini Tito?

Soma 1 Timotheo 4:12.

- Paulo alimshauri Timotheo nini?

Ni dhamira ipi ya jumla katika vifungu hivi vyote?

Tunahitaji kuwa kielelezo kizuri kwa wengine katika maisha yetu. Tunahitaji kuwaonyesha kwa maisha yetu jinsi ya kuwa Mkristo. Kuwa mfano ndio njia kuu ya kuwafunza wengine. Hatuwezi tu kutegemea mahubiri ya Jumapili kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

**SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Uliza swali lifuatalo na utengeneze orodha ya majibu kwenye ubao au karatasi. Hakikisha kikundi kinazingatia mambo kutoka maeneo yote 4 ya maisha. Acha kikundi kifikirie kile wanachoweza, lakini baadhi ya mawazo yametolewa hapo chini ili kukusaidia kuliongoza kundi katika kuzingatia maeneo yote ya maisha.*

Je, ni baadhi ya mambo gani ambayo waumini wapya wanapaswa kujifunza kufanya kwa njia ya Kiungu?

- Kuzingatia muda
- Kusimamia pesa
- Kuwapenda wenzi wao
- Malezi
- Kufanya maamuzi
- Kupenda jirani zao
- Kukabiliana na majaribu
- Kazi ya kila siku

Sasa angalia kila kitu kwenye orodha hii na ufikirie maswali yafuatayo:

- Je, haya ni mambo wengine wanayoweza kujifunza kwa kuangalia maisha yetu wenyewe? Kwa nini au kwa nini hapana?
- Je, sisi ni mifano mizuri ya mambo gani kati ya hayo? Tunahitaji kuboresha nini kati ya hayo?

## Kuwa Muwazi

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma 2 Wakorintho 3:4-6.

Kumfundisha mtu fulani haimaanishi kwamba tunapaswa kuwa wakamilifu kwanza. Ikiwa ni hivyo, hakuna anayeweza kuwafunza wengine kwa sababu hakuna aliye mkamilifu. Sisi sote hufanya makosa. Sehemu moja

ambayo watu wanaweza kujifunza kutoka kwetu ni kile tunachopaswa kufanya tunapokosea, kwa mfano tunapomuumiza mtu kwa maneno yetu.

Soma 2 Wakorintho 1:3-11.

Paulo alikabiliana majaribu mengi, hata hivyo aliwashirikisha wengine mambo haya (mstari 8).

- Baadhi ya sababu gani alizotumia kueleza kwa nini alikabiliana na majaribu hayo? (Mst 6,7)
    - *Walifarijiwa.*
    - *Wangekua katika ustahimilivu wanapokabiliwa na matatizo sawa.*

Hatupaswi kuogopa kushirikisha maisha yetu hata tunapohisi sio mazuri sana. Muumini mpya anahitaji kujua jinsi ya kushinda majaribu. Tunafundishwa kwamba katika maisha yetu ya Kikristo tutakabiliana na majaribu na tunapaswa kuwa na furaha kwa sababu ya hayo (Yakobo 1:2-3; 12).

Tukitaka kuwafundisha wengine tunahitaji wayaone maisha yetu. Hatupaswi kujaribu kujifanya kuwa sisi ni wakamilifu. Ni kwa jinsi gani mfuasi anaweza kukabiliana na majaribu na kutatua matatizo ya dhambi ikiwa hawatuoni tukikabili majaribu sawa au kutatua matatizo? Ndiyo, hii inaweza kutisha, kwa sababu utamaduni wetu unasema kwamba tunapaswa kuishi kana kwamba tunajua kila kitu. Lakini mfano wa mtume Paulo unatuonyesha kwamba hata viongozi wa Kikristo wanapaswa kushirikisha kuhusu mapambano yao.

**TAFAKARI NA MWENZAKO**

Pamoja na mwenzako, jadili maswali haya mawili:

- Unawezaje kuwa wazi zaidi katika maisha yako?
- Fikiria waumini wapya katika kanisa lako. Je, kuna mtu yeyote unayeweza kutumia muda naye na kuwa mfano wao wa kukufuata?

# Somo la 10: Kumletea Mungu Utukufu

**Mawazo Makuu**

1. Kusudi la maisha yetu ni kuleta utukufu kwa Mungu.

**Nyenzo**

1. Mwongozo wa Mwanafunzi Hiari (MW): Kusudi la Mungu
2.

## Ukristo ni nini?

**KIKUNDI KIKOGO CHA MAJADILIANO** (MW)

Kuna mwelekeo wa hatari kanisani siku hizi kwamba watu wanafikiri Ukristo unatuhusu sisi. Lakini huu si ujumbe wa Biblia.

Katika vikundi vidogo, soma mistari ya Biblia na ujibu maswali.

### Kusudi la Mungu

**Mwanzo 12:1-3**

- Mungu alimbariki Abrahamu kwa kusudi gani?

**Kutoka 14:1-4**
(Isipokumbuki hadithi hii, soma sura nzima ili ujue zaidi kuhusu kile Mungu alichokuwa amefanya.)

- Kwa nini Mungu aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu?

**Ezekieli 36:22-30**

- Kwa nini Mungu anasema atafanya mambo haya yote katika kifungu?

Ni jambo gani kuu katika vifungu hivi vyote?

**TOA RIPOTI**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Sikiliza majibu kutoka kwa vikundi. Hakikisha wanaona jambo kuu la vifungu hivi vya Biblia - kwamba Mungu anataka kujiletea utukufu. Huu ni ujumbe wa Biblia.*

Kila tunalofanya linapaswa kuwafanya wengine wamwone Mungu wetu kuwa anayestahili kuabudiwa, Aliye bora na wa ajabu zaidi. Hatupaswi kujifikiria sisi wenyewe bali Mungu. Ni lazima tuishi kwa njia ambayo watu waone jinsi Mungu wetu alivyo na nguvu na kutaka kumwabudu.

## Shadraka, Meshaki na Abednego

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Kuna hadithi nyingi zinazoonyesha jinsi Mungu anavyotukuzwa lakini tusikilize moja ya hadithi hizi:

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Tumia ustadi wako wa kusimulia hadithi kusimulia hadithi ya Shadraka, Meshaki, na Abednego iliyopo katika Danieli sura ya 3. Fanyia mazoezi ili kuhakikisha umejumuisha sehemu zote kuu:*

*Sehemu kuu za kujumuisha unaposimulia hadithi:*

- *Nebukadneza alijijengea sanamu na kuamuru kila mtu aiabudu kila waliposikia muziki huo. Wale ambao hawakutii wangewekwa katika tanuru inayowaka moto.*
- *Shadraka, Meshaki na Abednego walikataa kufanya hivyo.*
- *Walipoulizwa kwa nini, walijibu kwamba hawakuogopa tanuru kwa sababu Mungu angewaokoa. Hata ikiwa Mungu hakufanya hivyo, hawakutaka kuabudu sanamu ya mungu wa uwongo ambayo mfalme alikuwa amesimamisha.*
- *Nebukadneza alikasirika kwa hasira. Aliamuru tanuru iweke moto mara saba kuliko kawaida.*
- *Shadraka, Meshaki na Abednego walitupwa kwenye tanuru. Tanuru hiyo ilikuwa ya moto sana kiasi kwamba mwali wa moto huo uliwaua askari waliowatupa ndani ya tanuru.*
- *Mfalme alipowaona watu wanne, na si watatu, wakizunguka motoni, bila kuwadhuru, akawaamuru watoke nje.*
- *Baada ya hayo, Nebukadneza alimsifu Mungu na kutoa amri ya kuwakataza watu wa taifa lolote au lugha yoyote kusema lolote dhidi ya Mungu wa Shadraka, Meshaki na Abednego.*

**MASWALI YA KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

- Katika hadithi hii kilitokea nini?
- Mungu alitukuzwa jinsi gani?
    - *Katika sehemu ya kwanza ya hadithi, Nebukadneza alitaka kila mtu amwabudu. Mwishoni mwa hadithi alitambua kuwa ni Mungu ambaye ndiye Mungu wa pekee wa kweli na alimwabudu.*
- Jambo gani liliwatokea Shadraka, Meshaki, na Abednego?
    - *Walitupwa kwenye tanuru lakini Mungu akawaokoa*

Mungu alimtumia Shadraka, Meshaki, na Abednego kujiletea utukufu katika hadithi hii. Hata hivyo, walikumbana na jaribu kubwa. Wakati fulani Mungu huturuhusu kukabiliana na majaribu makubwa ili tuweze kumtukuza. Jambo la Shadraka, Meshaki, Abednego kukabiliana na mfalme na kujua kwamba wangetupwa ndani ya tanuru lingeweza kuwavunjika moyo. Walimtumaini Mungu kabisa, hata walipokabiliana na hatima mbaya inayoweza kutokea. Hatujui ni aina gani ya matatizo makubwa yatakuja tunapotafuta kumtukuza Mungu, lakini hata mambo yanapokuwa mabaya, tunahitaji kumtii.

## Kuakisi/kuonyesha Utukufu wa Mungu

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Soma 2 Wakorintho 3:18.

- Hutupata nini tunapoona utukufu wa Mungu?
    - *Tunabadilika.*
- Unadhani ni kwa nini?
    - *Ili tuweze kuangazia utukufu wa Mungu kwa wengine na kuwaonyesha wengine jinsi Yeye alivyo mweza yote, wa ajabu na mtakatifu.*
- Tunawezaje kufanya hili litendeke?
    - *Wote tunaweza kufanya ifanyike tunapotumia katika maisha yetu masomo ambayo tumejifunza kufikia sasa.*

**TAFAKARI NA MWENZAKO**

Je, umewahi kukutana na mtu yeyote aliyeonyesha utukufu wa Mungu kwako, ikimaanisha kwa kuwa karibu nao tu ulianza kumpenda Mungu zaidi? Mara nyingi hii ni kwa sababu ya jinsi wanavyowatendea wengine, jinsi wanavyozungumza, au hadithi wanazoshirikisha kuhusu Mungu akifanya kazi maishani mwao.

Na mwenzako, shirikisha kuhusu mtu katika maisha yako anayekuhamasisha kama hivi. Mtu huyo ana kitu gani kinachoakisi utukufu wa Mungu na kukutia moyo? Unaweza kujifunza nini kutoka kwao?

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Fikiria na kukumbuka masomo yote ambayo umejifunza hadi sasa. Ni mambo gani unaweza kufanya ili kumletea Mungu utukufu? Andika orodha ubaoni au kwenye karatasi.

- Wapende majirani zako, hata wale ambao ni vigumu kuwapenda.
- Jenga ufalme wa Mungu katika nyanja zote za maisha.
- Kuhudumia wahitaji.
- Tumia kile ulicho nacho ili kujenga Ufalme wa Mungu
- Fanya kazi kwa bidii.
- Kujali uumbaji.
- Tafuta na utumie kweli ya Mungu.
- Fanyeni wanafunzi.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Sikiliza majibu na ongezea majibu yaliyotolewa hapo juu wakikosa mojawapo. Tumia mjadala huu kuhakikisha kuwa kikundi kinakumbuka mambo makuu kutoka katika Somo la 1-10 kabla ya kuendelea na somo lifuatalo.*

# Somo la 11: Tufanyaje Mambo Haya Yote?

**Mawazo Makuu**

1. Tunahitaji kumtegemea Mungu.
2. Mungu anakusudia tuishi kama jumuiya, na kama mwili mmoja. Hatupaswi kuishi tofauti na kujitegemea kabisa kutoka kwa kila mmoja.

**Nyenzo**

Hakuna

## Utangulizi

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Inaonekana kwamba katika wiki chache zilizopita tulifanya orodha ndefu ya kile tunachopaswa kufanya. Hii inaweza kutufanya tujihisi kuelemewa.

Soma Mathayo 11:28-30.

Katika mistari hii ("Chukueni nira yangu mjifunze kwangu"), neno 'nira' lina maana ya 'kufundisha'. Yesu alisema hivyo mara tu baada ya kufundisha mlimani. Tukisoma Mahubiri ya Mlimani, tutaona kuwa si rahisi kufanya mazoezi. Zaidi ya hayo, sisi si wakamilifu (Mathayo 5:48).

- Kwa nini Yesu alisema ni rahisi kufanya ("nira yangu ni laini")?
    - *Kwa sababu kamwe hakupanga tuifanye peke yetu.*

Soma Yohana 15:1-8

- Nani ni mzabibu?
- Nani ni tawi?
- Tukikaa ndani yake kinatokea nini?
- Tusipokaa ndani yake kitatokea nini?
- Ni nani hutukuzwa tunapokaa ndani yake?

**KIKUNDI KIKODGO CHA MAJADILIANO**

Katika vikundi vidogo, jadili maana ya "kukaa" ndani ya Yesu. Tunawezaje kufanya hivyo? Tengeneza orodha ya njia mbalimbali.

**TOA RIPOTI**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Wape vikundi muda wa kujadili na kisha sikiliza majibu yao. Hapa kuna baadhi ya majibu yanayowezekana:*

- *Nenda kuabudu pamoja na kanisa*
- *Omba*
- *Tumia muda na Mungu.*
- *Soma Biblia*
- *Tafuta msaada kutoka kwa Mungu.*

# Kitabu cha Matendo

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Matendo ni kitabu kizuri. Yesu alifufuka na alikutana na wanafunzi na kuwapa Agizo Kuu (Mathayo 28:18-20). Wanafunzi walijua kwamba agizo hili haliwezekani kutekelezeka. Baada ya Yesu kufufuka, kulikuwa na watu 120 tu waliokusanyika kati yao. Watu hao wachache waliwajibika kufundisha mafundisho haya yote mapya kutoka kwa Yesu. Jamii iliyosalia ya Israeli walikuwa wamejaribu kusimamisha mafundisho yake. Isitoshe, Yesu alikuwa amesulubiwa hivi karibuni, kwa hiyo huu ulikuwa wakati hatari kwa Wakristo. Wanafunzi walikuwa na kazi kubwa mbele yao, na bado hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na ujuzi au elimu maalum (Matendo 4:13).

Soma mistari ifuatayo. Waumini walikuwa wakifanya nini katika kila aya?

- Matendo 1:14
- Matendo 2:42
- Matendo 4:24
- Matendo 6:4
- Matendo 10:9
- Matendo 12:5 na 12
- Matendo 14:23
- Matendo 16:25
- Matendo 21:5
- Matendo 28:8

Walitegemea nguvu za Mungu na Yeye aliwasaidia. Ikiwa hujui kitabu cha Matendo, ni lazima upange wakati wako wa kukisoma. Mungu alifanya miujiza mingi na kanisa lilianza kukua kutoka 120 hadi maelfu ya watu katika miji mingi. Kumbuka kwamba Mungu alianza kufanya mambo haya na watu wa kawaida, wenye elimu ya chini. Mungu hakutumia watu wenye nguvu zaidi, wenye ushawishi mkubwa zaidi.

Soma 1 Wakorintho 1:26-31

- Mungu anamtumia nani?
- Kwa nini?
    - *Kwa hiyo hakuna awezaye kujisifu na watu wote watajua kwamba ni Mungu afanyaye mambo makuu.*

Soma Yohana 16:5-14.

- Kwa nini Yesu anasema kwamba ni kwa faida yetu kwamba anaondoka?
- Roho Mtakatifu atatusaidia kwa njia zipi?

Wanafunzi walihuzunika kwamba Yesu alikuwa anaenda zake. Lakini ilikuwa kwa heri kwamba aliondoka, ili aweze kumtuma Roho Mtakatifu badala yake. Ikiwa Yesu angebaki duniani angekuwa mahali pamoja tu, na hata tungesafiri njia yote kwenda kumwona tusingeweza kupata muda wa kuzungumza naye peke yake pamoja na wengine wote ambao pia wangemtafuta kibinafsi. Lakini Roho Mtakatifu anaweza kuwa nasi sote, popote tulipo wakati wowote. Roho Mtakatifu daima yuko tayari kutuongoza na kutuongoza tukiomba. Anaweza kutusaidia kushinda magumu na majaribu. Hatuhitaji kukutana na changamoto peke yetu.

- Hii ina maana gani kwetu katika maisha yetu ya kila siku?
- Ni kwa njia gani tunaweza kuishi kwa nguvu za Roho Mtakatifu?
    - *Kuwa mtu wa maombi*
    - *Soma Biblia mara kwa mara ili kuelewa kile Mungu anachofundisha.*
    - *Tuombe Mungu atusaidie na atuongoze. Kumbuka kwamba anataka kushiriki nasi katika kazi zetu zote.*

# SEHEMU B:
# Kipengele cha 1: Tumetoka Mbali Kiasi Gani?

**Mawazo Makuu**

1. Sherehekea maendeleo yetu na fikiria mambo mengine tunayotaka kuyabadilisha.

**Nyenzo**

1. Vionyeshi: Kitini cha Mabadiliko ya Kawaida (nakala 1 kwa kila kikundi)
2. Mwongozo wa Mwanafunzi ni wa Hiari (MW):
    a. Jumuiya Iliyobadilishwa
    b. Mabadiliko ya Kawaida
3. Karatasi na Makapeni za kuchorea ramani

## Tumetoka mbali kiasi gani?

**MJADALA WA KUNDI KUBWA**

Soma Zaburi 145:6-7 and Nehemia 8:12.

- Je, mistari hii ina uhusiano gani?
    - *Inazungumzia sherehe - kusherehekea mambo mema ambayo Mungu amefanya na kusherehekea maarifa ya neno la Mungu.*

Fikiria miaka 5-6 iliyopita.

- Ni baadhi ya mabadiliko gani makubwa yaliyotokea katika jumuiya hii tunayopaswa kusherehekea?
- Mungu alibarikije?

**MJADALA WA KIKUNDI KIDOGO** (MW)

Baadhi ya makanisa yamebadilika sana.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Soma hadithi ya Jumuiya Iliyobadilishwa, kisha mkae katika vikundi vidogo na mjadili maswali mwishoni.*

**Jumuiya Iliyobadilishwa**

Hii ni hadithi ya jamii halisi. Mwaka wa 2005 watu wengi katika jumuiya hii walikuwa maskini. Nyumba zao zilikuwa rahisi na kuta za udongo, sakafu za udongo na paa za majani. Mashamba yalikuwa takriban kilomita 2 kutoka kijijini njia nyembamba za kutembea. Magonjwa yalikuwa kawaida na hali ya usafi ilikuwa mbaya. Hakukuwa na vyoo na wanyama hawakufungwa bali walitembea kwa uhuru katika jamii. Nyumba zingine zingekuwa na uzio kwenye milango ili kuzuia wanyama wasiingie ndani lakini wanyama walikuwepo kwenye uwanja ambao watoto walicheza. Watoto wachache walienda shuleni; wengi waliacha shule kwa sababu shule ilikuwa mbali sana. Kiwango cha juu zaidi ambacho mtu yeyote angeweza kusoma kilikuwa darasa la 9 kabla ya kwenda wilaya nyingine kuendelea na shule. Watoto wengi kwa kawaida walisoma kwa miaka michache tu.

Wakati huo hawakuwahi kufanya mradi wowote pamoja. Ikiwa mtu waliyemjua na kumpenda alikuwa mgonjwa basi wangemtembelea na kuleta zawadi za kimsingi za maziwa na sukari. Licha ya kufahamu mahitaji mengi katika jamii yao, hawakuwahi kumsaidia mtu yeyote zaidi ya familia na marafiki zao.

Siku moja watu wachache kutoka katika jamii walialikwa kuhudhuria mafunzo. Katika mafunzo hayo walijifunza kwamba Yesu hakufa ili tu waweze kwenda mbinguni, bali alikufa ili kurejesha mambo yote. Pia walijifunza kuwa wanahitaji kukua katika maeneo yote 4 (ya kimwili, kiroho, kijamii na kiakili) na kwamba wanahitaji kuwa tayari kutoa na kutumia kile walicho nacho. Wale waliohudhuria mafunzo hayo walirudi na kuanza kuwafundisha wengine kanisani mambo waliyojifunza.

Wale waliohudhuria mafunzo walitambua kwamba kulikuwa na wengi waliokuwa na uhitaji, lakini hawakuwahi kujaribu kuwasaidia watu hao kwa sababu hawakuwa marafiki au familia. Walianza kutoka kibinafsi na kusaidia wale waliohitaji msaada katika jamii. Kwa kawaida, walifanya mambo rahisi kama vile kuleta chakula kwa wazee au wagonjwa.

Takriban miezi 6 baadaye walijiunga na programu ya TCT. Baada ya mafunzo ya TCT waliunda Kamati ya Huduma katika Nyanja zote (WMC) kanisani na walianza kukutana kila wiki ili kujadili matatizo waliyoyaona katika jamii. Hawakuona tena baadhi ya watu kuwa Wakristo na wengine wasio Wakristo, lakini walizingatia ni nani wa kuwasaidia kwa msingi wa mahitaji yao. Katika kila mkutano wangejadili mahitaji waliyoyaona katika wiki iliyopita, kuchagua tatizo na kujaribu kusaidia familia hiyo. Msaada ungetofautiana. Ikiwa familia inaumwa sana kulima au kuvuna shamba lao basi timu kutoka kanisa ingeenda kufanya hivyo. Ikiwa nyumba ya mtu ilikuwa imeanguka au haikufaa kwa kuishi basi wangejenga nyumba mpya. Kwa miradi mingi ya awali wanachama wa WMC walichangia kwa kiasi kikubwa. Kiasi kilichohitajika kilikuwa kidogo sana. Mara nyingi wangetumia rasilimali zilizopatikana kwa urahisi.

Wanajamii walishangaa walipoona kile kanisa lilichokuwa likifanya na kuuliza kwa nini walikuwa wanasaidia. Waliwashirikisha kwamba “Katika Biblia Yesu anatufundisha kwamba tunahitaji kuwajali na kuwapenda jirani zetu. Mungu alitupenda na tunahitaji kuonyesha upendo huo kwa wengine.” Watu walikubali na wengi walianza kuhudhuria kanisani na kuwa Wakristo. WMC iliendelea kutumia muda wao kutafuta fursa za kusaidia na kuhusisha kanisa zima katika kusaidia.

Miezi michache baadaye walipata mafunzo ya pili. Kama sehemu ya mafunzo haya iliwalazimu kuchora ramani ya jumuiya yao kama walivyoota kwamba ingekuwa katika muda wa miaka 10-20. Katika ramani hiyo walichora shule, nyumba za matofali na saruji, barabara za mashamba yao na mashine za shambani.

Kikundi kiliendelea kukutana kila wiki lakini walipokutana wangeomba pia kwamba Mungu awaonyeshe ni hatua gani za kwanza wangeweza kuchukua ili kufanya ramani yao kuwa kweli. Wakati huo walikuwa na njia nyembamba za kutembea tu kuelekea mashambani mwao. Ndoto yao ilikuwa kwamba wangekuwa na mikokoteni ya kubebea mazao yao. Walipokuwa wakiomba walihisi kwamba wangeweza kujenga barabara za maeneo yao ya kilimo. Walitambua kwamba mambo waliyokuwa wakiota hayatashuka tu kutoka angani, bali walihitaji kuwa tayari kufanya kazi kwa bidii na kuomba kwamba Mungu abariki jitihada za mikono yao.

Wakakusanya kila mtu aliyekuwa tayari kusaidia na kuanza kupanua moja ya barabara iliyokuwa inaelekea mashambani. Kwa sababu kanisa tayari lilikuwa na sifa nzuri ya kusaidia katika jamii watu kadhaa walikuwa tayari kujitokeza kusaidia. Mradi huo ulichukua wiki chache kukamilika. Ilipokamilika walikuwa wamepanua njia ya kutembea hadi upana wa 1.5m. Barabara ilikuwa na urefu wa kilomita 2 hivi. Mwaka uliofuata walikamilisha barabara tano zinazozunguka jumuiya yao.

Baada ya kupanua njia ya kwanza, walinunua mikokoteni ya bei nafuu na kuanza kubeba mazao yao kupitia njia hiyo. Wengine katika jamii waliwaona na kuanza kuwaiga. Siku moja walipokuwa wakikutana mtu mmoja alishirikisha kwamba jumuiya nyingine ilikuwa na mkokoteni uliokuwa umefungwa kwenye pikipiki na kuvuta

mazao yao kupitia njia hiyo. Walifanya kazi pamoja kujaribu kuunda muundo ambao ungewaruhusu kufanya vivyo hivyo. Waliomba hekima na waliona kwamba Mungu aliwasaidia kuwa na mawazo.

Watu wa kanisa hilo waliendelea na miradi mingi kama ujenzi wa barabara, visima, vyoo, nyumba na mengineyo. Wale waliokuwa kanisani walifurahi sana kuweza kufanya miradi hiyo kwa sababu waliona ni njia ambayo waliweza kumwabudu na kumtumikia Mungu.

Lakini bado jamii ilikuwa na mahitaji kadhaa na walitamani kufanya miradi mikubwa zaidi ambayo ingemtukuza Mungu zaidi. Wangekusanyika kuomba na kumuuliza Mungu wafanye nini tena. Waliamua kujenga daraja. Ulikuwa mradi mkubwa na wa gharama kubwa na hawakuwa na uhakika kabisa jinsi ambavyo wangeweza kuufanya. Kufikia wakati huu baadhi ya viongozi wa serikali walikuwa wameshakuwa Wakristo na walipata msaada wa serikali na ahadi ya nondo kwa mradi huo. Walishiriki maono yao na waliokuwa kanisani na wengi walitoa pesa au kujitolea kusaidia. Hatimaye, waliona ulikuwa wakati mwafaka wa kuanza. Hawakuwa na nyenzo zote ambazo wangehitaji lakini waliamua kuanza hivyo hivyo. Walipoanza watu wengi zaidi katika jamii waliona kilichoendelea na wangejitolea kusaidia au kuleta pesa. Kila siku zawadi za vifaa na pesa ziliwatosha kuendelea. Hatimaye daraja lao lilikamilika.

Hata hivyo, mnamo Septemba 2009 dhoruba kubwa ilisomba daraja hilo. Licha ya ukweli kwamba kila mtu alikuwa amepoteza sana, walikusanyika pamoja kujenga daraja la muda. Kisha dhoruba nyingine kubwa ilipiga mnamo Novemba 2009 na kulibomoa. Tena, walikusanyika na kutengeneza daraja kubwa zaidi, lililo imara. Watu walitoa ardhi ili waweze kujenga katika eneo salama zaidi na kila mtu alichangia alivyoweza kuwa na vifaa. Serikali ilifurahishwa sana hadi ilialika kituo cha televisheni cha eneo hilo kuja na kurekodi kanisa lililoendelea kuipenda jumuiya yao. Habari hiyo ilionyeshwa nchini kote.

Wakati huo walikuwa wakipokea mafunzo zaidi. Kila baada ya miezi 4-6 wangepokea mafunzo mapya yakilenga zaidi ujuzi waliohitaji. Moja ya mafunzo yalikuwa juu ya afya. Baada ya mafunzo hayo walitambua miili yao walipewa kutoka kwa Mungu na wanapaswa kuitunza. Walielewa kuwa haikuwa kawaida kuwa mgonjwa wakati wote. Kama sehemu ya mafunzo walikuwa na masomo 20 ya vikundi vidogo kuhusu usafi na kutibu magonjwa ya kawaida. WMC ilikutana na kuamua kila moja ya vikundi vidogo vilipokutana kanisani (kama vile kikundi cha wanawake na vijana) wangejumuisha somo la afya baada ya somo la Biblia. Watu kanisani walipojifunza masomo ya afya waliyatumia katika maisha yao. Majirani zao waliona walichokuwa wakifanya na wao pia wakatumia masomo. Sasa kila mtu katika jamii ana choo na anatumia, huosha mikono yao kabla ya kula na kupika, huwafungia wanyama wao, huosha vyombo vyao na kuweka nyumba safi. Kila mtu ana nguo zinazofaa ambazo huziweka safi. Kila nyumba ina bustani ya mboga na familia sasa wanakula mboga. Sasa watu wanaumwa kwa nadra na wanaweza kujitibu isipokuwa kwa ugonjwa mbaya.

Mafunzo mengine yalikuwa juu ya ndoa na familia. Katika mafunzo hayo walijifunza majukumu ya mke na mume - kwamba mume anapaswa kumpenda mke na mke kumheshimu mume. Waume waliacha kuwapiga wake zao. Mwanamume mmoja alishirikisha kwamba hajawahi kumpenda mke wake. Ilikuwa ndoa iliyopangwa na hakumpenda haswa. Hakuwahi kumpeleka popote wala kumuonyesha mapenzi yoyote. Wote wawili walikuwa na huzuni. Baada ya mafunzo aligundua jinsi alivyokuwa akimtendea mkewe si sahihi. Biblia iliamuru ampende mke wake hivyo akaanza kumtendea mke wake mema. Sasa, alishirikisha, wana ndoa yenye furaha na wanapendana sana. Wanafurahia kuwa pamoja na kufanya mambo mengi pamoja.

Kanisa pia limebadilika sana. Kabla ya watu wengi walihudhuria mara kadhaa. Sasa kila mtu amejitolea kwa kanisa; hawahudhurii tu ibada ya kawaida ya kanisa bali vikundi vidogo pia. Wanasoma Biblia zao na zaka pia imeongezeka.

Kanisa bado linakumbuka siku, miaka mitano iliyopita, walipochora ramani. Ilionekana kama ndoto isiyo ya kweli kufikiria katika miaka 10-20 wangefanikisha kila kitu cha kwenye ramani. Lakini sasa wanapoitoa wanagundua kuwa ndani ya miaka 5 tu tayari wanayo yote. Sasa wana lori na wameboresha barabara hadi lori

linaweza kupita. Wana mashine za kilimo pamoja na trekta ya kawaida la kulima mashamba yao. Pia wana kiwanda karibu na jamii yao ina maana kwamba wanaweza kuuza mazao yao kwa bei ya juu zaidi. Wana shule na zahanati ya afya na kila mtu ana nyumba ya matofali yenye sakafu ya simenti. WMC inaendelea kukutana lakini sasa miradi wanayopanga ni kwa ajili ya jamii zinazowazunguka kwani hawana tena mahitaji katika jumuiya yao.

- Kilitokea nini katika eneo hili?
- Walifanya mambo gani tofauti?
- Walifanyaje?

**TOA RIPOTI (ikiwa unatumia vikundi vidogo)**

Huu ni mfano wa Kanisa lililotumia kile walichojifunza kwenye mafunzo. Walijaribu kadiri wawezavyo, wakajitolea sana, na Mungu akawasaidia. Mabadiliko yanaweza kutokea katika jumuiya zozote zinazotafuta msaada wa Mungu na kumtii. Ikiwa sio hadithi yako sasa basi unahitaji kuamua ikiwa unataka iwe yako katika miaka 2 au 3. Je, uko tayari kufanya kazi kwa bidii ili jambo hilo litokee?

## Mabadiliko ya Kawaida

**MJADALA WA KUNDI KUBWA**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Angalia orodha ifuatayo ya Mabadiliko ya Kawaida. Soma kila hoja kwa sauti na waambie washiriki wafikirie kama mabadiliko hayo yametokea katika jumuiya yao, si kabisa, kidogo, zaidi ya kidogo, au mengi. Kwa kila hoja waambie wanyooshe mikono yao kulingana na kiasi gani mabadiliko yametokea:*

- *Hakuna Mabadiliko - kunja ngumi*
- *Mabadiliko kidogo tu - inua mkono usawa wa bega*
- *Zaidi ya mabadiliko kidogo - inua mkono usawa wa kichwa*
- *Mabadiliko mengi – inua mkono kabisa hewani.*

*Waombe kila mshiriki kuendelea kuinua mkono wake kulingana na wanachofikiri kwa kila hoja moja. Andika vidokezo karibu na kila hoja kwa muhtasari wa majibu.*

### Mabadiliko ya Kawaida

**Kimwili**

- Kuboresha Afya
  - Kujenga na kutumia vyoo
  - Kuwa na maji safi na visima
  - Kuzuia na kutibu magonjwa ya kawaida
  - Kulima mboga na kula chakula chenye lishe
  - Kutumia shimo la takataka na kutupa takataka kidogo
- Kuongeza Kipato
  - Barabara bora au madaraja
  - Mifumo iliyoboreshwa ya umwagiliaji
  - Kuongezeka kwa faida kutokana na kupanda
  - Kupunguza deni na kusimamia bajeti vyema.
  - Kusaidiana badala ya kulipia kazi kama hapo awali.
- Makazi thabiti

**Kijamii**

- Ndoa Bora

    - Kuelewa majukumu ya mume/mke.
    - Kupatanisha familia zilizovunjika
- Ujuzi wa malezi ulioboreshwa
- Jamii hufanya kazi pamoja
- Uhusiano na mamlaka za serikali umeboreka

**Kiroho**

- Idadi ya waumini wanaokwenda kanisani iliongezeka
- Watu zaidi hushiriki katika mafunzo ya Biblia
- Fungu la kumi limeongezeka
- Watu zaidi hushiriki katika Matendo ya Upendo au njia zingine za kuwahudumia wengine
- Kupungua kwa migogoro ndani ya kanisa na kati ya makanisa
- Waumini waliojitolea zaidi
- Kuongezeka kwa uinjilisti kwenye maeneo magumu

**Kiakili**

- Kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaokwenda shule
- Kuongeza ujuzi wa:
    - Afya
    - Fedha
    - Kilimo
    - Biblia
    - Ujuzi wa kuwalea watoto

**Mengine**

- Mungu hutukuzwa - jumuiya, serikali na maeneo yanayozunguka wanajua kwamba Mungu ndiye sababu ya mabadiliko kati ya watu na jamii na anastahili utukufu.
- Kanisa linajua jinsi ya kuleta majaribu na changamoto kwa Mungu ili kutafuta suluhu. Kanisa ni aminifu kwa Mungu na huona jinsi Yeye ni mwaminifu katika kutimiza ahadi zake.
- Kanisa linaweza kuleta mabadiliko kwa jamii zinazozunguka.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Kwa sehemu ya mwisho (Nyingine) tazama kama kanisa lina hadithi zozote nzuri za kushirikisha kama mifano ya kila hoja.*

## Kutumia Yale Tuliyojifunza

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Kitini cha Mabadiliko ya Kawaida kinataja tu mambo ambayo kwa kawaida yametokea kupitia programu ya TCT. Pia kuna mambo mengine mengi ambayo tumejifunza kupitia mafunzo.

Fikiria tena kwa kila moduli ya mafunzo ya ujuzi (iliyoorodheshwa hapa chini) na ujaribu kukumbuka baadhi ya masomo na mawazo tofauti, hasa yale ambayo hayajatajwa katika Mabadiliko ya Kawaida. Je, kuna mawazo yoyote ya ziada kutoka kwenye moduli za mafunzo ya ujuzi ambazo zimetumika katika jumuiya yako? Andika vidokezo kwenye kitini cha Mabadiliko ya Kawaida cha mambo ambayo umeyaona au unayotaka kuona zaidi.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Hakikisha unafahamisha vizuri mafunzo haya ili uweze kusaidia kikundi kuyakumbuka.*

- Afya
- Ndoa na Malezi
- Usimamizi wa fedha
- Kilimo (Kupanda na Kufuga)
- Uinjilisti

## Tunataka kwenda wapi?

**MJADALA WA KIKUNDI KIDOGO**

Katika hadithi ya Jumuiya Iliyobadilishwa ***(Mwongozo wa Mwanafunzi)***, tuliambiwa kwamba watu katika jumuiya walikuwa wamechora ramani, kisha wakakusanyika ili kuomba mwongozo wa Mungu na kuamua jinsi wanavyoweza kufanya kazi ili kuona mambo yakitendeka.

Katika vikundi vidogo vya watu 4-6, omba na jadili ni mabadiliko gani unayotarajia kuona katika jumuiya yako siku zijazo. Tumia Kitini cha Mabadiliko ya Kawaida na mjadala uliopita kuhusu moduli za mafunzo ili kukusaidia kutambua mambo muhimu zaidi. Kisha chora ramani mpya ya miaka 5-10 ijayo ikionyesha:

- Mabadiliko unayotarajia kuyaona katika jumuiya yako.
- Jumuiya zingine ambazo unazotarajia kuzifikia

**TOA RIPOTI**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Baada ya vikundi kumaliza ramani zao, wawasilishe ramani zao kwenye kikundi kikubwa. Kisha uliza maswali yafuatayo:*

- Ni mambo yapi yanafanana kwenye ramani ya kila mtu?
- Kulikuwa na tofauti zipi?

Kwa kutumia mawazo haya, kwa pamoja sasa chora ramani moja unayoweza kutumia kama kanisa. Jaribu uwezavyo kuchora vizuri uwezekanavyo. Unaweza kumwomba mtu aliye hodari katika kuchora acjore ramani kwa kutumia mawazo yote makuu na kisha kuining'iniza kanisani ili watu waitazame mara kwa mara.

# Sehemu B: Kipengele cha 2: Kusonga Mbele

**Mawazo Makuu**

1. Tengeneza mpango wa jinsi ya kutimiza malengo yetu kama Kanisa la Ufalme

**Nyenzo**

1. Vionyeshi: Kadi za Sehemu za Mwili kutoka Moduli ya 2 - Ufalme wa Mungu
2. Karatasi na maka peni.
3. Kadi tupu
4. Mwongozo wa Mwanafunzi Hiari (MW): Kuandaa Mafunzo Mapya

## Sehemu zote zimeunganishwa pamoja

**MJADALA WA KUNDI KUBWA**

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Tumia* ***VIONYESHI****: Kadi za Sehemu za Mwili kutoka Moduli ya 2 – Ufalme wa Mungu kwa shughuli inayofuata. Onyesha kadi na uulize kikundi kama wanakumbuka walichojifunza kwenye somo la Moduli ya 2.*

Soma 1 Wakorintho 12:14-20.

- Fikiria kuwa mwili wako haukuwa na nusu ya viungo hivi. Je, mwili wako ungeweza kufanya kazi vizuri kama unavyofanya sasa?
- Kitatokea nini ikiwa mwili wako umepoteza 20% tu ya viungo, lakini bado ulikuwa na 80% ya viungo vya mwili? Je, mwili wako utaweza kufanya kazi vizuri?

Tunahitaji viungo vyote vya mwili vifanye kazi vizuri ili kuwa na ufanisi zaidi. Kila mmoja wetu ana jukumu la kujenga Ufalme wa Mungu. Hii inamaanisha sio tu viongozi ni muhimu, lakini kila mshirika wa kanisa ni muhimu. Majukumu yetu yanaweza kuwa tofauti, lakini jambo muhimu zaidi ni kwamba tunahitaji kutekeleza jukumu letu vizuri; kama sivyo, mwili wetu wa kanisa utakosa kile unachohitaji na hautaweza kufanya kazi vizuri.

Soma Waefeso 4:15-16.

- Kuna matokeo gani kila sehemu ya mwili inapofanya kazi vizuri?

Haya ni maono yetu - mwili wa kanisa wenye afya ambao kila mtu anashiriki katika kufanya mapenzi ya Mungu na kujenga ufalme wa Mungu kwa upendo. Tukitaka kweli kuona hili likitokea, tunahitaji kuweka mpango kama kanisa jinsi tutakavyoendelea kukua. Kuna sehemu 3 muhimu za kuzingatia:

1. **Mafunzo** - Washirika wote wa kanisa letu wataendeleaje kukua katika maarifa na uelewa?
2. **Matendo ya Upendo** – Tutaendeleaje kuonyesha upendo wa Mungu kwa jamii yetu na jamii zituzungukazo?
3. **Kukaa ndani Yake** – Tutatafutaje kukaa ndani ya Kristo na kumtegemea kama mwili mzima wa kanisa?

## Mafunzo

**KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO**

Katika Somo la 9 - Kuwafunza Wengine, ni baadhi ya njia gani tulizojifunza tunazoweza kuwafunza wengine?

Makanisa mengi yanaripoti kuwa yamekua kutokana na programu ya TCT huku watu wengi wakija kwa Kristo na waumini wengine wakianza kuhudhuria mara kwa mara. Mungu asifiwe! Hata hivyo, ni muhimu kwamba waumini hawa wapya na washirika wa kanisa pia wajifunze maana ya kumtii Mungu katika nyanja zote za maisha. Kuna njia mbili tunazohitaji kufanya hili - kufanya kazi pamoja na kufundisha.

**Kufanya kazi pamoja -** Ni muhimu sana kuwajumuisha waumini wapya katika kufanya Matendo ya Upendo kama kanisa. Hii ni mojawapo ya njia bora za kuwasaidia kukua katika imani na utii.

- Waumini wapya wangapi na washirika wa kanisa wamejiunga na kanisa lako katika miaka 5 iliyopita?
- Wanafunzwa kwa njia zipi kwa sasa?
- Je, wanashiriki mara kwa mara katika Matendo ya Upendo yanayofanywa na kanisa? Kwa nini?
- Unawezaje kuwasaidia kushiriki zaidi?

**MJADALA WA KIKUNDI KIDOGO**

**Kufundisha** ni njia ya pili tunayoweza kuwafunza waumini wapya na washirika wa kanisa. Hii ni msaada hata kwa washirika wa muda mrefu wa kanisa waliokosa mafunzo ya TCT.

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Andika orodha ifuatayo ubaoni ya baadhi ya Moduli za Mafunzo ya TCT.*

- Utangulizi wa Huduma Jumuishi.
- Ufalme wa Mingu
- Ukweli wa Mungu na Uongo wa Shetani
- Afya
- Ndoa na Malezi
- Usimamizi wa Fedha
- Kilimo (Kupanda na Mifugo)

Katika vikundi vidogo, angalia orodha na jadili maswali haya:

- Ipi kati ya hizo zimeleta matokeo makubwa katika kanisa lako?
- Ni ipi kati ya hizo mada unafikiri inaweza kusaidia kufundisha tena katika kanisa lako?
- Ni makundi gani katika kanisa lako yangefaidika zaidi kutokana na mafunzo haya?
    - *Mifano - kikundi cha vijana, kikundi cha wanawake, kikundi cha wanaume, waumini wapya au washirika wapya wa kanisa, vikundi vya kujifunza Biblia, Shule ya Jumapili, nk.*

**TOA RIPOTI**

**MJADALA WA KUNDI KUBWA**

Kumbuka kwamba SEHEMU A ya mafunzo haya ina masomo ya saa 1 unayoweza kufundisha kwa urahisi kanisani kwako kwa vikundi tofauti. Masomo haya yanajumuisha mambo muhimu zaidi kutoka kwa Moduli 1-3.

Afya, Ndoa na Malezi, Usimamizi wa Fedha, Kilimo (Kupanda na Mifugo), na Uinjilisti yote ni Mafunzo ya Ujuzi. YAnafundisha ujuzi wa msingi sana. Kanisa lako likielewa ujuzi huu wa kimsingi, basi uko tayari kujifunza zaidi. Kwa mfano, kanisa lako likitekeleza ujuzi wa kimsingi wa afya, basi wanaweza kufaidika kutokana na daktari kuja kufundisha maarifa ya ziada ya afya. Au kama tayari wanafanya kilimo, wanaweza kutaka mafunzo mengine ya jinsi ya kukuzalisha zao jipya la kibiashara. Baadhi ya watu wanaweza kufaidika na mafunzo ya biashara ndogo ndogo, au mafunzo mengine ya stadi za kujikimu kimaisha.

- Ni mafunzo gani mapya ya ujuzi yatayokuwa ya manufaa kwa kanisa lako? Orodhesha ubaoni.
- Kwa kila aina ya mafunzo yaliyoorodheshwa, fikiria ni nani unaweza kumwomba kutoa mafunzo hayo?

- Je, unawafahamu wataalam wowote kama madaktari, washauri nasaha, au wataalam wa kilimo?
- Je, Mashirika yasiyo ya kiserikali yoyote yaliyo karibu nawe au ofisi za serikali za mitaa hutoa mafunzo?
- Je, kuna mtu yeyote unayeweza kuwasiliana naye anayeweza kujua kuhusu mafunzo yanayopatikana?

***Maelekezo ya Mwezeshaji:*** *Soma juu ya Kuandaa Mafunzo Mapya. Hakikisha kikundi kinajiamini kwa jinsi wanavyoweza kumwendea mtu wa nje au kikundi kuomba mafunzo.*

### Kuandaa Mafunzo Mapya (MW)

Wataalamu wa nje na mashirika mara nyingi hutaka kujua kwamba kutoa mafunzo kutakuwa matumizi mazuri ya muda na jitihada zao. Wanataka kujua kuwa mafunzo yatapangwa vyema na kuna uwezekano wa kuwa na matokeo mazuri ya mafunzo hayo. Hapa kuna vidokezo vichache vya kushawishi vikundi vya nje kuwa ni wazo zuri kuja kutoa mafunzo katika kanisa lako:

1. **Shirikisha baadhi ya hadithi kuhusu kanisa lako jinsi lilivyo hai katika jumuiya.** Hakikisha unajumuisha hadithi zinazoonyesha manufaa kwa jamii nzima na si washiriki wa kanisa lako pekee. Hii ni muhimu hasa ukimwomba mtu asiye Mkristo au kikundi kuja kutoa mafunzo. Watataka kujua kwamba kushirikiana na kanisa kutakuwa na matokeo chanya kwa jamii nzima.

2. **Eleza ni nani utamchagua kuhudhuria mafunzo na kwa nini.** Wataalamu wa nje na mashirika wanataka kujua kwamba watu wanaohudhuria mafunzo yao watakuwa watu wanaofaa zaidi kwa mafunzo hayo. Kwa mfano, huwezi kutoa mafunzo ya uvuvi kwa kikundi cha wakulima, au mafunzo ya uongozi ikiwa viongozi wa kanisa lako hawawezi kuhudhuria. Unataka kuchagua watu watakaotumia vyema na kushirikisha kile wanachojifunza. Mashirika mengi yanathamini kujua umefikiria mambo na kuwa na mpango ulio wazi. Wanaweza pia kuwa na mapendekezo fulani lakini ni vizuri ikiwa umeshatayarisha baadhi ya mawazo ya kuwasilisha.

3. **Kujipanga vizuri.** Uwe na mtu mmoja anayewajibika kuwasiliana mipango kwa uwazi kwa mtu wa nje au kikundi. Waombe washiriki kufika kwa wakati. Kuwa na nyenzo zozote za mafunzo zinazohitajika, au chakula au vinywaji vilivyoandaliwa mapema. Tukio lililopangwa vizuri litaleta hisia nzuri kwa mtaalam wa nje, na watakuwa na shauku kubwa ya kutaka kufanya kazi nawe siku zijazo.

**Tengeneza Mpango**

Kama kikundi kikubwa, tengeneza orodha ya malengo yanayowezekana kwa mafunzo ambayo ni muhimu zaidi kwa kanisa lako kupokea katika miaka 2 ijayo. Hizi zinaweza kuwa moduli za TCT zinazorudiwa au mafunzo mapya ya ujuzi. Bainisha ni makundi gani katika kanisa yangefaidika zaidi na kila mafunzo. Ukimaliza, jadili au upigie kura malengo ambayo ungependa kutimiza ndani ya miaka 2 ijayo. Tengeneza bango linaloorodhesha malengo haya. Jadili kwa ufupi nani ana jukumu la kuandaa kila mafunzo.

## Matendo ya Upendo

**SHUGHULI YA KIKUNDI KIKUBWA**

Angalia ramani uliyochora ya jumuiya yako na jumuiya jirani. Ni mabadiliko gani yote uliyotaka kuyaona yakitokea katika siku zijazo? Andika kila moja kwenye kadi. Je, kuna mabadiliko yoyote unayotarajia kuyaona ambayo bado hayajaorodheshwa?

Panga kadi katika mafungu: muhimu zaidi, muhimu, sio muhimu sana. Kwa kadi zilizo muhimu zaidi weka alama tatu kwenye kadi. Kwa kadi zilizo muhimu weka alama mbili. Kwa kadi zisizo muhimu sana weka alama moja.

Ziweke kadi pamoja tena na uzipange kulingana na jinsi shida ilivyo rahisi kutatua. Rahisi kutatua, rahisi kidogo, na ngumu sana kutatua. Kwenye kadi ambazo ni rahisi kutatua weka alama tatu, kadi za rahisi kidogo weka alama mbili na vigumu kutatua weka alama moja.

Tafuta kadi zote zilizo na alama 6 (au alama 5 ikiwa hakuna kadi zilizo na alama 6.) Hizi ndizo kadi zilizo muhimu zaidi na rahisi kutimiza. Tengeneza bango lingine linaloorodhesha mabadiliko haya.

**KIKUNDI KIDOGO CHA MAJADILIANO**

Katika vikundi vidogo, ombeni pamoja na kisha mjadili - Ni Matendo gani ya Upendo kanisa lako linaweza kufanya ili kufanyia kazi mabadiliko haya?

**TOA RIPOTI**

Muda ukiruhusu, chagua Tendo moja la Upendo na upange wakati wa kulifanyia kazi.

## Kukaa ndani Yake

Katika Somo la 11 tulizungumza jinsi tunavyoweza kutimiza mambo haya yote. Jibu lilikuwa nini?

- Mtegemee Yesu na ukae ndani yake.

Soma Yohana 15:5.

Ingawa tumezungumza jinsi tunavyotumia hili katika maisha yetu ya kibinafsi, tunahitaji pia kuzingatia jinsi tunavyomtegemea Yesu kama mwili mzima wa kanisa.

- Ni kwa njia gani kanisa lako kwa ujumla linatafuta kumtegemea Mungu?
- Je, kila mtu anashiriki?
- Je, kanisa lako hukusanyika mara kwa mara ili kuomba na kufunga kuhusu matatizo ya jumuiya?
- Kama ni hivyo, umeona kikitokea nini kutokana na muda huo unaotumika kuomba na kufunga pamoja?
- Kanisa lako linaweza kufanya nini mwaka ujao ili kuanza kumtegemea Mungu zaidi?

**MAOMBI KATIKA KIKUNDI KIDOGO**

Angalia mabango hayo matatu - ramani mpya, malengo ya kufundisha, na orodha ya mabadiliko muhimu zaidi /rahisi. Tumia muda kuomba katika vikundi vidogo ili Mungu akusaidie kutimiza haya kwa utukufu wake. Baada ya kuomba, shirikisha mawazo yoyote mapya yaliyokujia na kikundi kikubwa.

## Hatua ifuatayo ni ipi?

Hongera! Umefikia sehemu ya mwisho ya mafunzo ya programu ya TCT. Fikiria juu ya njia zote kanisa lako na jamii zimebadilika na kukua katika miaka kadhaa iliyopita. Mungu ni mwema sana!

Mabango matatu uliyotengeneza ni zana za kukusaidia kuendelea kukua na kumtukuza Mungu. Tunapendekeza uyaweke katika kanisa lako kama ukumbusho wa mara kwa mara wa kuendelea kufanyia kazi malengo yako. Umeshafanikiwa mengi sana, na ukiendelea kumtegemea Mungu na kuwa mtiifu, basi yatatokea mengi zaidi.

Katika miaka michache ijayo tutaendelea kuwasiliana ili kutoa nyenzo za ziada za kujifunza. Tunatumaini mtaendelea kukutana pamoja na kufanya Matendo ya Upendo. Endelea kutumia yale Biblia inayofundisha katika sehemu zote za maisha. Endelea kutafuta hekima na usaidizi wa Mungu unapotaka kujua jinsi ya kuleta mabadiliko kwa jamii.